# *Tunutu, Nzige, Parare, Madumadu*

Asante, Ndugu Neville. Niliona waliendelea kusogeza hiki kipaza sauti kidogo, au kuongeza sauti. Mnaweza kunisikia vizuri? Hiyo ni sawa. Ninii . . . Asanteni.

Usumbufu huo kidogo, dakika chache tu zilizopita, ulikuwa, ndugu mmoja aliliegesha gari lake mahali pabaya hapa nje, nao watu, nadhani, wanataka alisogeze. Ndivyo ilivyokuwa. Na yeye . . .

[Ndugu Gene Goad anazungumza na Ndugu Branham kuhusu maikrofoni—Mh.] Hii *hapa*? Vipi kuhusu mimi kuleta hii huku? Mnaweza kunisikia vizuri? Mimi . . . Huo ni msemo wa Kentucky, "Tulikuwa tunabwekea kichaka kisicho." Nilikuwa nikitazama kwenye maikrofoni *hii*, na *hii* inapaswa kuwa ndiyo. Hiyo ni sawa. Asante, Ndugu Gene. Sasa, leo, ni . . .

2 Tuna furaha kutoa taarifa ya mkutano wa—wa Middletown, Ohio, juma lililopita, au juma kabla ya wiki jana, ndivyo lilivyo, sasa. Huo ulikuwa wakati mtukufu kwetu. Tulikuwa na . . . Loo, makusanyiko hayakuwa makubwa sana. Lakini ilikuwa huko bara mahali wanapopaita Chatauqua, huko mbali sana, maili nane ama tisa nje ya jiji. Lakini vi—viti vilijaa, na viliwaenea watu elfu chache. Sijui sana kuukadiria umati. Na kwa hiyo jambo kuu, lilikuwa, Yesu alikutana nasi, na hiyo ndiyo sehemu nzuri. Basi ilileta matokeo makuu, Ambaye tunampa sifa, Bwana Mungu, kwa kutufanyia haya.

3 Basi kulikuwako na baadhi ya watu wazuri sana niliopata kukutana nao maishani mwangu, katika nchi hiyo. Na kwa kuwa tuko karibu sana na mpaka hapa, huenda nikasema hivi, walikuwa asilimia tisini na tisa Wakentaki. Kila kitu kule juu kilikuwa Kentaki. Ndugu Sullivan alisema, "Ndugu Branham," akasema, "unajua, kote, karibu bonde hili lote dogo linalopitia hapa, ni Kentaki?"

Nami nikasema, "Si—sikujua hilo."

Akasema, "Ndiyo, ndivyo lilivyo."

4 Basi usiku mmoja mkutanoni ilitokea tu nilitaja, "Ni wangapi hapa wanatoka Kentaki, inueni mikono yenu." Nikaangalia pande zote, nikawazia, "Kuna mtu yeyote wa kutoka mahali pengine?" Wote ni moja kwa moja tu, Kentaki.

5 Nayo matokeo yalikuwa ya ajabu, ripoti nyingi sana! Kulikuwako na mu—muungwana mmoja, jana, ambaye alikuwa akipita, akapitia na kunieleza baadhi ya mambo yaliyokuwa

yametokea, na barua zinazoingia, na shuhuda mbalimbali. Na kisha kulikuwa . . .

6 Kuna bwana mmoja hapa nyuma anayerekodi sasa hivi, naye akasema, usiku fulani, naamini alisema "jana usiku," nilipokuwa nikihubiri juu ya yule tai mdogo. Naye akasema ya kwamba . . . Katika mstari wa upambanuzi, au labda ilikuwa katika kusanyiko, nisingesema ni wapi hasa, lakini kulikuwa na mtu aliyekuja kutoka kwa wasikilizaji. Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kuzungumza naye, na kumwambia kwamba yeye hakutoka nchi hiyo, bali alitoka Indiana, mahali fulani huko Indiana. Naye akasema kwamba, "Hujasimama hapa kwa ajili yako mwenyewe. Umesimama hapa kwa ajili ya mtoto wako mchanga, mwenye umri wa miezi michache tu, labda miezi mitatu," na kitu kama hicho. Naye alikuwa anaenda kufanyiwa upasuaji, na ilibidi moyo utolewe. Nayo ilikuwa ha—hali ya kusikitisha sana; maskini mapafu yake madogo yalikuwa yamevimba, kifua chake; tumbo lake dogo lilikuwa limesinyaa kabisa. Na kumwambia aende nyumbani, asione shaka; lakini kama asingetilia shaka, angemkuta mtoto wake mchanga akiwa mzima.

7 Sasa, shahidi yuko kwenye chumba hiki kingine hapa sasa, na labda huyo mtoto mchanga yuko kwenye hili kusanyiko, nijuavyo mimi. Mapafu ya huyo mtoto mchanga yakawa mazima, nalo hilo tumbo dogo likapona. Naye mtu anayerekodi humu ndani, moja ya kanda asubuhi ya leo, akamleta mama, baba yake, na nanii wake . . . jirani ya mtu huyu anayenasa kanda, basi akawaleta humu ndani, kisha akamleta huyo mtoto mchanga, na kumlaza huyo mtoto mchanga chumbani, kisha akaicheza kanda, iliyokuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Naye akasema walipofika mahali pale ambapo huyo muungwana alikuja kujiwasilisha jukwaani, kasema, "Roho Mtakatifu aliingia chumbani, kwa kuwa hapo aliketi huyo mtoto mchanga papo hapo, akipiga kelele na kucheza, na kuendelea." Hakuhitaji upasuaji. Madaktari hawakuhitaji kufanya upasuaji. Bwana alimfanyia mtoto huyo upasuaji, kwa Nguvu Zake kuu, kuu kabisa. Naye maskini huyo mtoto mchanga ameketi pale, akicheza kwenye kitanda kidogo, na—nao mama na baba wameketi pale, na jirani ambaye inawezekana kidogo alishuku jambo hilo lote; huo hapo ule Uwepo. Ikiwa hiyo si imani ya kimitume, sijui ni nini.

8 Mnajua, Biblia ilisema, wakati Yesu alipokuwa, kupitia kwa mtume Petro na Yohana, alipokuwa amemponya yule kiwete langoni, "Wasingeweza kusema lolote dhidi yake, kwa sababu mtu huyo alikuwa amesimama hapo kama shahidi." Kwa hiyo, Kristo angali hai. Jina Lake lihimidiwe. Ni faraja jinsi gani siku hizi! Sasa, huo ni mmoja tu wa shuhuda nyingi. Lakini jinsi ilivyo siku hizi, kujua ya kwamba Mungu yule yule, pamoja na matendo yale yale ya ajabu, mambo yale yale aliyofanya,

anayafanya vivyo hivyo siku hizi, kwa sababu Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Tunashukuru kuwa na majaliwa ya kukusanyika asubuhi ya leo katika Jina Lake.

9 Sasa, tuombeeni tunaposafiri mahali mahali, kumtumikia Bwana katika nafasi ambayo Yeye atatuitia. Nasi tunafurahi ya kwamba hawatoki tu humu maskanini, bali wanatoka pande zote, nchini kote.

10 Asante, dada. Hilo lilikuwa ni jambo la uaminifu. Najua ya kwamba Mungu mkuu wa Mbinguni alikuona ukifanya jambo lilo hilo. Mama, mdogo sana kuliko mwingine, anayeketi hapa. Na ni mwanamke ambaye amekuwa hudumani kwa ajili ya Bwana, miaka mingi kabla sijazaliwa, yeye pamoja na mumewe; miaka hamsini na kitu, wakihubiri Injili. Yeye mwanamke akifanya kazi katika mgodi wa makaa ya mawe, apate kumsaidia mumewe hudumani, kuihubiri Injili ninayoitetea. Huyo mwanamke mkongwe alikuwa ameketi mbele, bila feni, akifuta jasho usoni mwake; msichana mmoja anaamka na kumletea feni yake. Kwa hiyo, ninawaambia, nina furaha kukusanyika asubuhi ya leo pamoja na watu kama hao, inanifurahisha kwamba mimi ni Mkristo, na nimekusanyika pamoja na Wakristo.

11 Sasa ni joto sana nchini mwetu, na kote nchini sasa. Nasi tunatarajia kuja kwa msimu wa kupukutika majani ambapo itakuwa baridi kidogo. Mkutano wetu mkubwa ufuatao tunaoujua uko San Jose, California. Huko ndiko tulikokuwa kwenye viwanja vya maonyesho kwa siku chache, na kulikuwa na mkutano mkubwa sana, hatungeweza hata kuwashughulikia. Na vikundi vivyo hivyo vinaifadhili mikutano ijayo sasa kwenye viwanja vya maonyesho huko San Jose. Nasi tunatumaini kwamba ikiwa unaishi karibu na huko, au marafiki, andika na uwaambie wauhudhurie huo mkutano. Msipouhudhuria, mtuombee.

12 Sasa, leo hii, nilitaja ya kwamba nilikuwa niwe hapa asubuhi ya leo, kujiunga katika maombi na katika dua kwa Bwana, pamoja na nyinyi watu wote. Na kukiweko na wageni kati yetu, tunasikitika kwamba jengo letu halijayoyozwa, bali sisi ni kanisa maskini tu, katika mali ya ulimwengu, lakini matajiri katika Imani katika Ufalme wa Mungu. Na tunawakaribisha kwa ziara hii fupi, tukiomba kwamba mtarudi na kuwa pamoja nasi tena. Siku moja tunatumaini kuwa na kanisa bora zaidi.

13 Hatuko sana kwenye miradi ya kujenga makanisa siku hizi, kwa sababu tunaamini kweli, kwa mioyo yetu yote, Bwana Yesu yuaja hivi karibuni. Na huku wamishenari wakiwa hudumani, wakiihubiri Injili, bila viatu, wakila mlo mmoja kwa siku, tunawezaje kujenga kanisa la dola milioni moja katika hali hiyo? Kamwe si—siwezi kuliona, na kisha kusema, "Bwana yuaja hivi karibuni." Hebu tuingie hudumani na kufanya tuwezayo katika

kizazi hiki. Kukiweko na kingine, hebu. . .Watawajibika kwa chao; itabidi tuwajibike kwa hiki. Kamwe siwezi kuyaendea majengo hayo ya dola milioni moja, na kadhalika, baada ya kuwa hudumani na kuona hilo.

14 Sasa, ni nzuri. Nafikiri nyumba ya Bwana inapaswa kuwa nzuri. Na inapaswa kuwa ma—mahali padogo patakatifu. Tupafanye pa kustarehesha na pazuri iwezekanavyo, lakini sio chochote kilichokiuka mipaka, kwa sababu hatuelewi hilo.

15 Sasa kabla hatujaomba na kusoma Maandiko, nilitaka kutoa. . .si kuhubiri asubuhi ya leo, bali kutoa hotuba juu ya Maandiko. Na kwa kawaida nikija. . .Mimi hufanya hili tu kanisani mwangu, na tuko kanisani mwetu. Sisi si dhehebu. Sisi ni wasiofungwa na madhehebu, asili yetu, wala hatujajumuishwa na makanisa yoyote ya mrengo wa madhehebu, lakini tunashirikiana na waaminio wote wa madhehebu yote na watu wote kote duniani. Kanisa letu dogo, asubuhi ya leo, linajulikana ulimwenguni kote. Kanda ambazo ninyi. . .Jumbe hizi, kadiri zilivyokatikakatika, hata hivyo tunasaidia, kwenye huduma za kimishenari, (ni mataifa mangapi tofauti ya kigeni?) mataifa kumi na tisa ya kigeni, kwa kanda pekee.

16 Mataifa kumi na tisa mbalimbali yanachukua hizi Jumbe na kuzitafsiri. Mtu fulani, ninapohubiri, mtu fulani anasimama pale akihubiri moja kwa moja pamoja nao. Nazo zinaingia kwenye vibanda na mahali ambapo Mungu hata hajulikani, na kuwahubiria makafiri, na kwa wenyeji wa Afrika na Marekani Kusini, na kote ulimwenguni, na mamia mara mamia wanamjia Bwana. Wengi wanaponywa. Na hiyo ndiyo sababu tunajisikia ya kwamba ni muhimu sana kuusukuma huu Ujumbe, sio katika majengo makubwa na kadhalika.

17 Na halafu wakati nikiwa hapa, ninatoa tu maonyo juu ya Maandiko. Lakini, huko nje hudumani, sihubiri Mafundisho yoyote ya kanisa, kwa sababu, kufanya hivyo, huifanya kuwa vigumu. Watu watasema "Mafundisho yangu si sahihi," au kitu kama hicho. Na kama ukihubiri moja. . .Kama nikihubiri fundisho la Kimethodisti, Wabaptisti hawatakubaliana nami. Kama nikihubiri la Kibatisti, basi Walutheri hawatakubali. Nikihubiri la Kipentekoste, basi Wanazarayo hawatakubali. Nikihubiri la Kinazarayo, basi church of God hawatakubali. Kwa hiyo, mnaona, unapaswa kuchukua msimamo kwa ajili ya jambo fulani, lakini, katika upeo wa huduma ya utumishi, tunamkaribisha tu kila mwaminio, haidhuru imani yako au dhehebu lako ni lipi. Maadamu umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, wewe ni ndugu na dada yetu. Nasi tunakusudia kuliweka hivyo sikuzote.

18 Na basi, Bwana akipenda, leo hii, nataka kuhubiri, katika kanisa letu, kanisa letu linasimama juu ya Fundisho la Biblia,

kile kanisa linachosimamia, na sababu ya sisi kufanya hivi. Na kufanya hivyo, hatuna budi kuunda au. . . hatukusudii hilo, lakini huenda tukazua maswali akilini mwa mtu, kusema, "Vema, kamwe sikufundishwa jinsi hiyo, wala kuliamini kwa njia *hiyo*." (Asante.)

19 Basi ikitokea ya kwamba utaninii. . . kanisa lako haliamini, ama wewe huamini mambo tunayozungumzia kama Fundisho la kanisa letu, tunatumaini kwamba kamwe halitakwaza. Kwa sababu, hatua yenyewe ya kwanza kabisa ya Ukristo wenye mafanikio, na kuonyesha kwamba mtu amempokea Roho Mtakatifu, ni unyenyekevu, unyenyekevu halisi uliotolewa na Mungu, ambao hauna budi kutolewa kwa unyenyekevu. Lakini, hata hivyo, kanisa lisilo na Fundisho ni kama tu kiwavi wa baharini; halina uti wa mgongo. Kwa hivyo, inatubidi tuwe na uti wa mgongo kwake. Wala si uti wa mgongo tena, lakini meno, pia, kwa sababu Kanisa la Mungu halina budi kula Mkate wa Uzima.

20 Nasi, katika baadhi ya matamshi ambayo huenda nikatoa, kama nikijaribu kulishindilia kwa nguvu, sasa naomba msilielewe vibaya. Kwamba, simaanishi kuwa fidhuli, katika kutoa maonyo juu ya Biblia. Lakini kama mimi, katika miaka thelathini ya kutafuta, pasipo kuchukua kanuni za imani wala chochote ila Neno tu. . . Kunao watu hapa ambao ni Wapresbiteri, Katoliki, Baptisti, Pentekoste, Nazarayo, church of God, Pilgrim Holiness, wote wameketi hapa. Nami ninajua ya kwamba kila kanisa lina kanuni zake lenyewe za imani, wala sitaki kupinga hilo, bali ninajaribu tu kuleta Maandiko na kulifanya kwa Maandiko. Hivyo basi wote—wote wataelewa kwamba sio kuwa fidhuli. Ni kuwa tu na upendo na mapenzi, na kwa rehema, na vizuri nijuavyo jinsi ya kuyaelezea Maandiko.

21 Na sasa hili somo asubuhi ya leo kidogo litakuwa somo refu, nami sitaki kuharakisha. Ninataka kuchukua wakati wangu kwa yale tu nitakayosema, na kujaribu kulielezea, ni kwa nini tunalisema.

22 Mara nyingi sana mikutanoni, mtu fulani atasema, "Vema, kwani yeye anaamini nini? Je, yeye ni Mbaptisti, bado? Yeye ni Mpentekoste? Anaamini katika kunena kwa lugha? Au, yeye ni wa *hili*, au *lile*? Yeye ni wa usalama wa Milele? Au, yeye ni nini?" Halafu basi utaje tu kitu chochote ulicho, wataanguka kama viazi moto. Haijalishi, hawatatulia wasikilize, wakazingatie, bali wataachana nawe upesi sana.

23 Hakuna mahali popote katika mikutano yangu, wakati wowote, nimewahi kujua nimeacha mafarakano miongoni mwa ndugu. Daima ninahubiri tu Kuja kwa Bwana, wokovu, na—na uponyaji wa Kiungu. Hilo halimuudhi mtu yeyote wa Injili Yote.

24 Halafu kanisani hapa, nina Fundisho letu wenyewe. Linapenya kati ya watu wanaokuja, na kusema, "Vema, mimi. . .

Ndugu Branham alisema *hivi na hivi*, mambo hayo." Vema, hatuna budi kuwa na Fundisho.

25 Sasa, hivi majuzi tu kwenye mkutano, wakati mtu fulani aliliuliza kundi la wahudumu. Makatibu wangu na hao wengine wakiwapo. Barua nyingi, nyingi sana ziliingia, na kusema, "Je, Ndugu Branham anaamini katika ku—kuhifadhiwa au kuwekwa, usalama wa mwaminio?" Vema, nilijua, katika kundi la washika sheria waliokuwa wakiuliza hilo, ingekuwa vigumu kwangu kusema hilo; wangesema "achaneni naye" haraka sana. Na hiyo haileti tofauti hata kidogo kama unaamini hilo au la; mradi tu umeokoka, hilo ndilo jambo kuu. Nami sikusema chochote. Ndipo makanisa kumi na sita mbalimbali yakasitisha ufadhili, mnaona. . . ati kwa sababu nilikataa kujibu, kwa sababu ya kudumisha ushirika na watu.

26 Sasa, kanisani asubuhi ya leo, nataka kuelezea ni kwa nini ninaamini ninayoamini.

Na tuombe.

27 Bwana, uliyemfufua Yesu katika wafu, na umemtoa kwetu kama Dhabihu ya pendo Lako kwetu, na kwa kuoshwa kwa maji kwa Neno, Yeye amewatakasa watu wa kipekee, kundi lililoitwa litoke, nasi tunangojea kwa subira Kuja Kwake mara ya Pili. Nasi tunajua ya kwamba, machoni pa watu, kuna kanuni nyingi za imani na madhehebu mengi. Na, Baba Mungu, tungeomba ya kwamba Wewe ungebariki kila mmoja wao. Na msimamo wanaouchukua, ingawa tunaweza kutokubaliana nao katika mambo mengi, hata hivyo, kimsingi, kama Wakristo na kama ndugu, tunasimama bega kwa bega pamoja nao. Na si tu bega kwa bega, lakini moyo kwa moyo. Katika siku ya kutojali, wakati watu ni wakaidi na wenye majivuno, wapendao anasa za ulimwengu kuliko kumpenda Mungu. Tunaomba, Ee Mungu, kwamba Roho Mtakatifu ataifunga mioyo yetu karibu zaidi, sote, siku baada ya siku. Waponye wagonjwa asubuhi ya leo, Bwana.

28 Kuna wale wanaopaswa kuingia katika ubatizo wa maji. Nasi tunaomba ya kwamba Roho Wako Mtakatifu atawajaza na (ule) Uwepo Wake kama bado hawajaupokea huo. Jalia watiwe muhuri mbali na mambo ya ulimwengu, na kujazwa na Roho wa Mungu, katika upendo wa Kiungu wa Mungu, na kwa ushirika pamoja na watu wote.

29 Bwana, chini katika mataifa ya ulimwengu, kama vile ulivyonituma, maskini mtu asiye na elimu. Na hata hivyo, Bwana, nikiamini moyoni mwangu, juu Yako, mambo ambayo nimeamini na kufundishwa na Biblia, na kuthibitishwa na Malaika wa Bwana Yule anayesimama hapa kuthibitisha yale yanayosemwa, kama ni ya Mungu. Mara nyingi, watu wameniwazia mimi kuwa mtu wa kupatana. Wewe ndiye hakimu wa moyo wangu. Lakini kama vile Paulo wa kale, ambaye

hata alihubiri dini ya Kiyahudi mpaka akawafanya watu kumwamini, ndipo basi akahubiri Kristo aliyesulubiwa; lakini kwanza kusudi watu wapate kumwamini, kusudi Ujumbe wake ukolee chumvi. Tunaomba, Ee Bwana, ya kwamba utakoleza mazungumzo yetu na ushirika wetu, kwa Chumvi ya Roho, kwa Damu ya Bwana Yesu, na utufanye watu walioitwa, na ili kwamba ulimwengu upate kutazama na kuyaangalia maisha yetu, ndipo upate kiu ya kuwa kama sisi. Utudumishe wanyenyekevu, na kujazwa na upendo na Roho Wako. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake Yeye aliyeomba kwamba tuwe kitu kimoja, ndipo, watu wote wapate kujua kwamba tulikuwa watoto Wake, tunapopendana mmoja kwa mwingine. Amina.

30 Sasa, kwenu, najua kidogo kuna joto. Basi kama kuna—kuna feni ya miguu hapa nyuma ambayo wanataka kuileta popote, ingeonekana ni bora, ni sawa. Ningependa tu kusoma baadhi yake sasa kutoka kwenye Maandiko Matakatifu.

[Ndugu Neville anasema, "Feni hii inakusumbua?"—Mh.] Hapana, bwana. Sio maadamu iko sakafuni namna hiyo. Ninaamini ingekuwa ni sawa, Ndugu Neville.

31 Nataka mfungue pamoja nami katika Maandiko, kwenye Kitabu cha Yoeli, halafu nina sehemu kadhaa hapa ambazo ningependa kusoma, kwanza, kupata maonyo, muktadha fulani kwa ajili ya maonyo. Kwanza, katika Yoeli, mlango wa kwanza, kuanzia kifungu cha kwanza, na kusoma cha 4. Na halafu katika mlango wa pili, cha 25 hadi cha 27, tutasoma kwa ajili ya somo la Maandiko.

> Tena *neno la* BWANA*. . .lilimjia Yoeli mwana wa Pethueli.*
>
> *Sikieni haya, enyi wazee, sikilizeni, enyi wenyeji wote wa nchi.* Je, *mambo haya yamekuwako katika siku zenu, au katika siku za baba zenu?*
>
> *Waarifuni watoto wenu habari yake, watoto wenu wakawaambie watoto wao, na watoto wao wakawaambie kizazi kingine.*
>
> *Yaliyosazwa na tunutu. . .yameliwa na nzige; na yale yaliyosazwa na nzige yameliwa na parare; na yaliyosazwa na parare yameliwa na madumadu.*

32 Na kisha katika kifungu cha 25 hadi cha 27, cha mlango wa pili.

> *. . .nitawarudishia hiyo miaka iliyoliwa na nzige, na parare, na madumadu. . .tunutu* na madumadu, lile *jeshi kubwa nililotuma kati yenu.*
>
> *Nanyi mtakula chakula tele, na kushiba, na kulihimidi jina la* BWANA*, Mungu wenu, aliyewatendea mambo ya ajabu: na watu wangu hawatatahayarika kamwe.*

*Nanyi mtajua ya kuwa mimi niko katikati ya Israeli, na ya kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu, wala si mwingine: na watu wangu hawatatahayarika kamwe.*

33 Halafu katika Kitabu cha Warumi, na katika mlango wa kwanza wa Warumi, na kifungu cha 25, ninasoma hili. Tutachukua cha 24, pia.

*Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika* unajisi wa *mioyo yao, waufuate uchafu, hata wakavunjiana heshima miili yao:*

*Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu* kuwa *uongo*. . .

34 Na halafu katika Warumi, mlango wa 3 na kifungu cha 4. Warumi 3, na mlango wa 4, tunasoma. Sehemu ya kwanza ya huo mlango wa 4.

*Hasha!*. . .*Mungu aonekane kuwa amin na kila mtu mwongo;*. . .

35 Sasa tunaingia kwenye wazo zito la masomo hapa. Na sasa sisi. . .Ninaamini kwamba utakuja wakati wa kurejeshwa kwa mambo yote ambayo yamefanywa vibaya. Na tunajaribu, kwa yote yaliyo ndani yetu, na watu wengine wanajaribu, wainjilisti wakuu kama vile Billy Graham na Oral Roberts, na wengine wengi wa wainjilisti mashuhuri, wahudumu, wachungaji, ambao ni waaminifu kwa wadhifa wao, wanajaribu kuona uamsho katika wakati wetu. Nanyi, watoto wa Mungu, mnaombea uamsho katika wakati wetu. Makumi elfu ya maombi hukutana na Mungu kila saa, kwa ajili ya uamsho katika wakati wetu. Na imeandikwa katika Maandiko, "Kama watu wanaoitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja, na wataomba, basi nitasikia kutoka Mbinguni." Sasa, ikiwa watoto wa Mungu wanakusanyika pamoja na kuombea uamsho katika wakati wetu, na uamsho hauji, basi hapana shaka kuna kasoro mahali fulani.

36 Sasa, kumbukeni, ya kwamba, kitu chochote kinaweza kufanya kazi tu unapotenda kazi katika kanuni ya kitu hicho. Nguvu za ulimwengu zinaweza kutenda kazi tu kulingana na kanuni za ulimwengu. Sayari zinaweza tu kusonga zinaposukumwa na kanuni za sayari. Jua linaweza tu kuchomoza kulingana na vile dunia inavyolizunguka jua. Na kwamba hapo, ni, kila kitu hakina budi kufanya kazi kulingana na kanuni za mpango wake. Kwa maana, Mungu aliumba vitu vyote, na kuweka kanuni kwa ajili ya kitu hicho. Na ndipo halina budi kuzunguka, na kufanya kazi, na kutekeleza mambo sawasawa na kanuni ya kitu hicho. Haitafanya kazi kwa usahihi kwa njia nyingine yoyote.

37 Hebu weka mnyororo kwenye jino la gurudumu, kisha uuweke kwenye kigingi cha mviringo. Huenda ukaweza kufanya majira kidogo. Lakini njia pekee ambayo utawahi kufanya

majira sahihi na mnyororo huo, ni kuweka jino la gurudumu ambalo ni sawa na hilo jino lililo nyuma yake, halafu hayo matundu madogo kwenye mnyororo huo yakutane, yaliyopimiwa wakati sawasawa na hilo jino, ndipo unaweza kwenda mahali fulani.

38 Nami nina hakika ya kwamba tuna jino baya mahali fulani. Kanisa linasonga polepole sana kwa ajili ya saa tunayoishi. Kuna kitu kimeenda vibaya kabisa. Na inatupasa sisi katika siku hii, katika kukaribia kwa Kuja kwa Bwana, kuketi chini na kusoma hili na kuona kuna shida gani, tutafute chanzo chake. Kamwe huwezi kupata tiba mpaka upate chanzo chake.

39 Kama daktari, kama ukiingia ofisini mwake na kusema, "Ninaumwa na kichwa, na kuumwa na tumbo," naye akupe aspirini ndogo, ama chochote kile, na kukuachilia, anajaribu tu kukuondosha. Daktari halisi, wa kweli, atakichunguza kisa hicho mpaka agundue ni kiungo gani kina shida, ndipo akishughulikie kiungo hicho.

40 Hivyo ndivyo ilivyo na Ufalme wa Mungu. Tunapaswa kujua kuna shida gani, kisha tuishughulikie hiyo. Maandiko ni kama maagizo ya daktari.

41 Daktari, wanasayansi wanaofanya kazi kwa bidii kupata dawa, pia, ya—ya kuua kijidudu fulani, ugonjwa ulio mwilini mwako, kama homa ya matumbo, au—au ugonjwa fulani, ambapo wanaweza kukupa seramu ambayo itaua chembechembe hiyo ya homa ya matumbo, na hata hivyo inabidi ishughulikiwe kwa uangalifu sana (. . .?. . .), ishughulikiwe kwa uangalifu sana, hadi hii: ikiwa haitoshi, haitasaidia mgonjwa; na ikiongezwa kitu kingine, huenda ikamuua mgonjwa. Inapaswa kutolewa na muuza dawa, kulingana tu na maagizo.

42 Kwa hiyo, kama kuna shida kanisani siku hizi, kwamba haliendelei jinsi ipaswavyo, ni maoni yangu kwamba tunapaswa kurejea kwenye yale Maagizo, tujue shida iko wapi hasa, hata kanisa hili ni wagonjwa sana kwamba kuna ugonjwa kanisani mwetu, ugonjwa wa dhambi. Kisha inatupasa kujua ni nini Daktari aliagiza, na tuone kama wauza dawa wachungaji wetu wanatupa Maagizo sahihi. Pia, kumbuka, unaweza kuongeza kitu fulani kwenye Maandiko yaliyobainiwa vizuri sana, na kumwua mgonjwa. Na labda, sisemi tumeongeza, lakini vipi kama baadhi ya wauza dawa wetu wameongeza kitu fulani kwenye Maagizo ya Mungu? Endapo wameongeza, wanamuua mgonjwa, wakiwaacha wafe katika dhambi.

43 "Vema, ni," unasema, "vema, kama walikuwa waaminifu!" Hapana, hiyo hailipatii udhuru.

44 Mtu, muuza dawa, alimpa mtu asidi kaboliki, hapa miaka michache iliyopita, mwaminifu tu kadiri alivyoweza kuwa, na ni mfamasia aliyesajiliwa, nayo ikamuua huyo mtu. Hata hivyo, alikuwa mwaminifu. Hakuna . . . Uaminifu, nimeona uaminifu

miongoni mwa makafiri, ambao ungeufanya uaminifu wa Kikristo uonekane kama kitu huko nyuma katika siku za kale. Nimewaona wapagani ambao wangewaweka watoto wao katika kinywa cha mamba, kumtoa dhabihu kwa mungu wa majini. Nisingeweza kupata uaminifu huo miongoni mwa Wakristo. Nimeona watu ambao wangejilaza kwenye misumari. Na kuvunja mifupa ya miguu yao wakiwa watoto wadogo; nimewaona wakiwachukua watoto wachanga na jamaa wadogo, na kuwakatakata na kuwatia alama, na kuwatoa damu, na wakati mwingine kuyachukua maisha yao. Uaminifu wenye kilindi, lakini wamekosea.

45 Sasa hebu tupate kitu fulani. Ayubu, au Yoeli, hasa, nilito-. . .nadhani alitupa msingi mzuri hapa. Na huo ndio tunaotaka kuchukua kwa ajili ya somo. Alisema:

> Ninyi waarifu—waarifuni *watoto wenu. . .watoto wenu wakawaambie watoto wao, na* wao wakawaambie wengine, na kadhalika, *kwa kizazi kingine,* ambacho kitakuwa ni Mataifa. Waambie Israeli waendelee kuyasimulia.

46 Na sasa Andiko hili ambalo Yoeli alinena habari zake limetimizwa leo hii wakati sisi, Wamataifa, tumelipokea. Alisema:

> *Yaliyosazwa na tunutu yameliwa na* madumadu;. . . madumadu, nzige, na kadhalika.

47 Nao wadudu hawa, ikiwa utachukua kitabu chako cha wadudu, utagundua kwamba wadudu hao wanne mbalimbali ni mdudu yule yule katika hatua nne mbalimbali za maisha yake. Sote tunajua kwamba ki—ya kwamba ki—kifukofuko si kingine ila ni madumadu aliyefunikwa, na ataangua kipepeo; naye kipepeo ni madumadu kabla hajaanguliwa. Tunutu, nzige, na kadhalika, ni kitu kile kile. Ni mdudu yule yule. Sasa chochote. . .

48 Sasa sikilizeni kwa makini. Chochote kilichotukia kwanza, kwa mdudu tunutu, alifanyika tu madumadu, baadaye. Naye madumadu akawa nzige, baadaye. Na chochote kile kilichoanza hapo mwanzo, kingali ni kitu kile kile kinachotatiza siku hizi. Basi hebu turudi sasa katika Maandiko tuone kilichoanza.

49 Sasa, tunajua ya kwamba tunaweza tu kujenga kanisa, kwanza, juu ya nyenzo ambazo Mungu alitupa kulijengea. Hizo tu ndizo tulizo nazo. Nami nadhani, kabla. . .Najua Hili ni kali, na liko kwenye kanda, mamia ya watu ulimwenguni kote watasikia. Lakini kabla hatujaweza kuwa na jengo la Kanisa la Mungu, itatubidi kurudisha vitu hivyo vyote ambavyo wadudu hawa wamekula Kwake. Itabidi turudi na kujua kile kilicholiwa na hao wadudu. Na mbele ya Mzabibu huu wa Bwana, Mzabibu. . .Yeye ndiye Mzabibu; sisi ni matawi. Na kabla hatujapata kujua, ama Kanisa halijaweza kusimama

katika nguvu zake rasmi na za asili, itabidi turudi nyuma tuone kilicholiwa na hao wadudu. Ndipo itabidi Kanisa hilo lirejeshwe hapo tena, la sivyo kamwe halitasimama katika nguvu zake na utukufu wa msimamo wake wa kwanza.

50 Ikiwa ganda litang'olewa kutoka kwenye mti, tunapaswa kulirudisha hilo ganda juu yake tena. Likuze hilo ganda, kwanza. Huwezi kupata matofaa mpaka ulikuze hilo ganda. Kwa maana, ganda ndilo mkondo wa utomvu. Mkondo wa utomvu ndio tegemeo la uhai.

51 Nayo Maandiko, Biblia Takatifu ya Mungu, ndiyo tegemeo la Uhai kwa kanisa lolote. Tungewezaje kamwe kuupitisha utomvu wa zabibu kwenye ganda la mkuyu? Kamwe haiwezekani. Inabidi tuwe na ganda la Mzabibu. Hatuna budi kuwa na lile ganda asili. Na kuna njia moja tu ambayo ganda hilo linaweza kurudi kwenye Mzabibu, ni wakati Mungu anapolikuza, Mwenyewe.

52 Hatuwezi kutengeneza baadhi yake na kuliweka juu yake. Halitafaulu. Hakuna mpango wa kujibunia utakaofanikiwa. Itahitaji njia ya Mungu la sivyo halitaishi kamwe. Mipango ya kujibunia haitafaa kitu. Unaweza kuuzungushia huo mti tambara, na kusema, "Acha ukue." Tambara halikuwa mpango wa Mungu. Inabidi liwe ni ganda, tegemeo la maisha, Ndipo unapotoka kwenye mizizi, utazaa maisha yale yale ambayo huo mti ulikuwa nayo kabla haujaliwa na hao wadudu.

53 Si ajabu hatuwezi kufanya miamsho ya uponyaji. Si ajabu makanisa yamefarakana. Si ajabu mtu atasema, "Loo, *hili*, *lile*, na *linginelo*," ubishi chungu nzima. Si ajabu kuna itikadi kama hizo kati yetu, ni kwa sababu hatuwezi kuzaa matunda halisi ya saburi, uvumilivu, wema, upole, unyenyekevu. Mkondo wa Uhai umekatwa kutoka kwenye huo Mti, nasi hatutawahi kuileta kupitia kanuni za imani za tambara au ganda lingine lolote lililowekwa mahali pake. Itachukua nguvu za Mwenyezi Mungu kuukuza mti huo uirudie hali yake tena.

54 Hivi Yesu hakusema, nayo Maandiko yamesema, "Wana macho wala hawawezi kuona, wana masikio wala hawawezi kusikia"? Kamwe hawawezi kusikia. Wala hakuna mtu anayeweza kuja kwa Mungu, ama kwa Kristo, mpaka Mungu amfunulie.

55 Hivi majuzi nilikuwa nikizungumza, nasi tulikuwa tukiyawazia Maandiko. Nikasema, "Ni kwa nini watu hawawezi kuona Hilo?" Nikasema, "Hilo hapo," ndipo ikatokea niliwazia. Sijali ni dhahiri jinsi gani, jinsi Maandiko yanavyolifundisha, kamwe hutaweza kuliona mpaka Mungu Mwenyewe akuonyeshe Hilo; sijali ni dhahiri jinsi gani. Nayo Biblia nzima imejengwa, na Kanisa lote la Mungu aliye hai, limejengwa juu ya ufunuo wa kiroho wa Neno. Kwa nini Habili akatoa dhabihu iliyo bora

kuliko ya Kaini? Kwa nini Habili hakumfuata Kaini; alikuwa na kanisa zuri kuliko yote? Lakini ilifunuliwa kwake.

56 Yesu alipokuja kutoka Mlima wa Kugeuka Sura, nao wakasema . . .

"Watu husema Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?"

57 "Mmoja akasema 'Eliya,' na mmoja akasema Wewe ni 'yule nabii,' na kadhalika."

Akasema, "Lakini ninyi mnasema Mimi ni nani?"

Petro akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

58 Akasema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza jambo hilo kwa vitabu fulani, ama kwa seminari fulani, ama kituo fulani cha taratibu za kujibunia. Lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hilo, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda." Haya basi, ufunuo wa kiroho wa Neno la Mungu.

59 Katika Mathayo 11, ninaamini ndipo, ama 12, mahali fulani hapo, imeandikwa, ambapo lilisema, "Ingawa Yesu alikuwa amefanya miujiza mingi sana, ishara nyingi sana ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, hata hivyo watu hawakuweza kuamini hilo. Kwa sababu Isaya alisema, 'Wana macho wala hawawezi kuona. Wana masikio wala hawawezi kusikia.'" Vipi? Ingawa walikuwa wasomi, ingawa walikuwa wanadini wakuu sana; walikuwa watakatifu, na bila kosa wala lawama. Kama walipatikana na yodi moja ya makosa, walipigwa mawe, bila huruma. Hakuna mtu angaliweza kuweka kidole juu yao. Walisoma Maandiko, mchana na usiku, kizazi baada ya kizazi, na bado Mungu alikuwa ameyapofusha macho yao.

Mnasema, "Ati Mungu akawapofusha?" Hivyo ndivyo alivyosema.

60 Mungu hufanya atakacho. Hatuwezi kumwambia la kufanya. Hivi Paulo, katika Kitabu cha Warumi, mlango wa 8, hakusema ya kwamba, "Mungu alimwinua Farao na kuufanya moyo wake mgumu, akayapofusha macho yake, kwa kusudi lili hili, ili mapenzi Yake yatimizwe"? Na Esau je? Na Yakobo . . . Esau, alikataliwa, kabla huyo mvulana hajazaliwa; Mungu alimdharau. Unaona, yote yanafanya kazi kulingana na uteuzi mkuu wa Mungu kimbele. Yeye halali. Anajua vizuri kabisa.

61 Na tunawahukumu watu kulingana na ninii yao . . . inavyoonekana, uaminifu wao au unyofu wao. Tunayahukumu makanisa kulingana na maendeleo yao. Tunajiunga, tunawachukua wainjilisti, kwa sababu kwamba wao ni wakuu. Hivyo sivyo.

62 "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe."

63 Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu. Kuna kasoro fulani, mahali fulani, maana Neno la Mungu ni la Milele kama vile Yeye alivyo wa Milele. Wala Neno la Mungu haliwezi kushindwa kama vile Mungu asivyoweza kushindwa, Mwenyewe. Sasa, kuna kasoro, mahali fulani.

64 Kwa hiyo hebu turudi nyuma sasa. Msingi ambao sasa tumeuweka. Hebu turudi nyuma, tuchukue somo letu la Warumi 3:4, "Neno la kila mtu na liwe uongo, nalo Neno la Mungu liwe Kweli."

65 Nitawaelewesha hili barabara, nami ninawatakeni msikilize. "Na iwe ni Mungu, Ukweli." Hebu tujiweke sawa na yale Mungu aliyosema, bila kujali mtu mwingine yeyote alisema nini. Ninataka kutumia mambo manne mbalimbali ya yale ninayoona katika Maandiko, ambayo wadudu hawa wamekula kutoka katika Kanisa la Mungu aliye hai, na kuulemaza Mzabibu wa Mungu, ama kuudumaza.

66 Tutakubali, ninyi Wamethodisti mtakubali, ninyi Wabaptisti mtakubali, ninyi Wapresbiteri, ninyi Wapentekoste, ninyi Nazarayo, nyote mnakubali, maskani hapa inakubali, "Kuna kasoro fulani." Nasi, maskani, tuna hatia tu kama hao wengine, kwa kuwa, "Yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi."

67 Sasa hebu turudi nyuma. Nami nataka kutaja mambo manne, Kimaandiko tu kadri nijuavyo kuwa, ambayo wadudu hawa wamekula kutoka Kanisani, kutoka kwa hali Yake ya kwanza, ya asili.

68 Sasa, jambo la kwanza, kanisa lilianzishwa kwenye Siku ya Pentekoste. Petro alihubiri ma—mahubiri ya uzinduzi kwenye ile ibada ya kwanza, wakati Kanisa lilipozaliwa. Kanisa la Kikristo lilizaliwa kwenye Siku ya Pentekoste. Na kama Mungu hana kikomo, hana kikomo, wala hawezi kubadilika, Kanisa Lake halina budi kubaki kama lilivyokuwa hapo mwanzo. Je, mnakubali hilo? Kanisa halina budi kubaki kama lilivyokuwa.

69 Bali mwanadamu ameliingilia ovyoovyo, wakaweka tafsiri zao wenyewe ndani Yake. Kamwe usijaribu kulifasiri Neno la Mungu. Sema tu kile Hilo lisemacho. Haijalishi jinsi lilivyo, kwa hiyo ambatana tu na Hilo, hivyo tu. Usilibadilishe Neno. Biblia ilisema, kwamba, "Maandiko si ya kutafsiriwa apendavyo mtu kibinafsi." Hatuna haki ya kusema mambo haya; inatubidi tu kulisoma na kusema jinsi tu lisemavyo, na kuliamini vivyo hivyo. Sijali jinsi linavyoonekana la kijinga; liamini, kwa vyovyote vile.

70 Mimbara si mahali pa mzaha. Ni mahali pa uaminifu. Simaanishi hili kutania. Namaanisha hili kunukuu kitu nilichoambiwa. Kasema, kulikuwa na ndugu mzee mweusi kule kusini, aliyeibeba Biblia, naye bosi wake alikuwa akimdhihaki. Akasema, "Huwezi kuisoma; kwa nini kuibeba?"

71 Alisema, “Ninaibeba kwa sababu ninaiamini.” Hiyo ni sababu nzuri. “Siwezi kuisoma, lakini ninajua kuna kitu fulani ndani Yake. Ni ya kweli.” Kasema, “Ninaamini hata ‘chalada’ iliyo upande Wake wa nje. Imeandikwa ‘Biblia Takatifu’ juu yake. Ninaiamini.”

72 Akasema, “Chochote ambacho Biblia hiyo ingesema kifanywe, nadhani ungekifanya?”

73 Akasema, “Ndiyo, bwana. Ukilisoma kutoka katika Biblia, nitafanya hivyo iwapo ni Amri ya Mungu.”

74 Akasema, “Basi vipi kama nilisoma kutoka katika Biblia hiyo, na kukuambia Bwana alisema uruke kupitia ukuta ule pale, ule ukuta mkubwa wa mawe? Ungewezaje kamwe kuruka kupitia ule ukuta wa mawe kama hakuna shimo ndani yake?”

75 Akasema, “Kama ulisoma hayo kutoka kwenye Biblia, naye Bwana aliniambia niruke, Yeye angekuwa na shimo pale wakati nikifika pale.” Na hiyo ni kweli.

76 Mungu akisema hivyo, haidhuru linaonekana kuwa ni la kipuuzi jinsi gani, wewe piga hatua juu ya Hilo. Ni juu ya Mungu kuyashughulikia hayo mengine, hiyo ni kazi Yake. Ni kazi yako kupiga hatua.

77 Sasa moja ya mambo ya kwanza ambayo ningependa kuwazungumzia kwa dakika hizi chache. Baada ya kupata kuwa msingi hauna budi kuwa wa asili, hauna budi kurudi kwenye msingi, hauna budi kurudi pale ulipokuwa ni Mzabibu. Ikiwa una kasoro, nao huo Mzabibu haufanyi kazi vizuri, hebu turudi nyuma tuone kuna shida gani.

78 Sasa, moja ya mambo ya kwanza ambayo ningependa kutaja, ni kwamba kitu fulani kimetoka kanisani mwetu, moja ya mambo makuu, ni Imani. Watu hawana Imani siku hizi kama waliyokuwa nayo katika siku zile. Namna fulani ya parare, wa namna fulani, ameingia na kula kutoka mkondo wa Uhai wa Imani. Waliibadilisha. Siku hizi imani yao inategemea aina fulani ya—ya kanisa kubwa la kimadhehebu. Lakini Yuda alitwambia, katika Yuda kifungu cha 3. Ilisema:

> *Wapenzi,* . . .*nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu, niliona ilifaa kuwaandikia* . . .(Ninayo hapa mbele yangu.) . . .*ili niwaonye kwamba mwishindanie ile imani* (sio imani fulani; *ile* Imani) *waliyokabidhiwa watakatifu mara moja.* (Hiyo ilikuwa ni miaka thelathini na mitatu kabla ya hapa, walikabidhiwa Imani hii.)

79 Sasa, siyo . . .Watu wanasema, “Loo, hiyo ni kinyume na imani yangu.”

Kuna Imani moja tu. “Bwana mmoja, Imani moja, na Ubatizo mmoja.” Unaweza ukawa na imani *fulani*, lakini tunataka *ile*

Imani. *Mwishindanie kwa bidii*, hiyo ni kusema, “mwitetee,” kusimama, “mwisimamie.”

> . . .*mwshindanie kwa bidii imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*

80 Ni lini walipoitwa watakatifu? Walipotakaswa. Roho Mtakatifu aliwatakasa. Wakaitwa watakatifu. Sasa Yuda anasema, ndugu, ndugu wa kulea wa Yesu, “Ninawatakeni mwishindanie kwa bidii ile Imani iliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. Kamwe msiiache Imani hiyo ianguke.”

81 Nayo Imani ya watakatifu haikuwa katika kanuni za imani, si katika madhehebu, si katika majengo ya kanisa, si katika mashirika, bali ilikuwa katika Uwepo wa Mungu aliye hai. Walikuwa na Imani ya kuwaponya wagonjwa, kuwatoa pepo, kufanya miujiza. Ahadi zote kuu ambazo Yesu alitoa, kanisa hilo la kwanza lilizishikilia Hizo. Ilikuwa ndiyo mkondo wa Uhai.

82 Sikilizeni hapa. Sikilizeni kwa makini yale ninayotaka kuwaambia. Uwepo udumuo wa Mungu aliye hai ndio mkondo wa Uhai wa kanisa lolote ama kundi lolote la watu, Uwepo udumuo wa Mungu aliye hai kutenda kazi, na kufanya, na kutekeleza, na kuishi pamoja na watu kama Yeye alivyofanya hapo mwanzo. Ikiwa Uwepo wa Mungu aliye hai ulileta pentekoste yenye nguvu, pamoja na ishara, na maajabu, ukaleta watu waliojawa sana na Utukufu wa Mungu sana hata wakapiga makelele na kunena kwa lugha zingine, nao wakaenda na kuifia ile Imani, hebu na tuishindanie kwa bidii Imani hiyo hata kifo kitakapotuweka huru. Ishindanie kwa bidii. Hatutapatana, juu ya kusoma vitabu, kuchukua theolojia fulani iliyobuniwa na mwanadamu. Hatutapatana, juu ya kanuni fulani za imani ama vitabu fulani vya maombi, ama jambo fulani ambalo mtu mwingine amesema.

> Imani yangu haijajengwa juu ya kitu kingine
> Ila Damu ya Yesu pamoja na haki;
> Kila kitu karibu na nafsi yangu kikitoweka,
> Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na ngome yangu.
>
> Kwa kuwa kwake Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;
> Sakafu zingine zote ni mchanga unaodidimia.

83 Hakuna kanuni ya imani ila Kristo, hakuna sheria ila upendo, wala hakuna kitabu ila Biblia. Hakuna vitabu vya kanuni ya imani! Biblia haina budi kusema hivyo. Biblia haina budi si kulisema tu, bali kulisema kila wakati vile vile, haina budi kulisema kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Haina budi kuingia katika kila utando mdogo, na kupenya katika kila sehemu ya Neno. Isipofanya hivyo, basi nina tafsiri mbaya Yake, maana Mungu hawezi kulipinga Neno Lake Mwenyewe. Lisiposema jambo lile lile kwa kila unyuzi mdogo!

84 Ikiwa shati hili hapa, limefumwa lote kwa unyuzi ule ule, ndio unaolifanya kile lilicho. Ndio unaolifanya jeupe.

85 Hivyo ndivyo Kanisa lilivyo. Kama litakuwa Kanisa jeupe, lililozaliwa mara ya pili, lisilo na waa, lisilo na kunyanzi, halina budi kufumwa kwa aina ile ile ya uzi lilioanza nao, kwenye Siku ya Pentekoste, ujuzi wa Roho Mtakatifu, ukichoma na kufuma. Huwezi kuongeza kipande cha kitambaa kilichooza. Huwezi kuongeza kipande cha gunia la turubai kwake. Halitafaa kitu. Litaliharibu.

86 Namna fulani ya maskini parare wa kale ameingia na kuila Imani hiyo. Wanasimama na kusema, "Ninaamini katika kanisa takatifu. Kanisa takatifu la Katoliki ya Kirumi, ninaliamini."

87 Ninamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Ninaamini Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na Imani na Nguvu za kufufuka Kwake zinaishi ndani yangu leo hii. Kwa kuwa Yeye yu hai, mimi ni hai pia. Si kwa sababu ya kanuni ya imani, si kwa sababu ya madhehebu; bali kwa sababu Kristo yu hai. Nami niko ndani ya Kristo, ninaishi kwa Yeye, na pamoja Naye, nami ninaishi kupitia Yeye. Na Uhai Wake unajipenyeza Wenyewe kwangu. Usipopitia humo, basi siwezi kujiita Wake. Yeye hachukui tu kichwa changu; huuchukua moyo wangu, mienendo yangu, kila kitu changu, na kujipenyeza Mwenyewe ndani yake.

88 Anajipenyeza Mwenyewe katika Neno. Neno haliwezi kusema jambo moja, mahali pamoja, na jambo lingine mahali hapa pengine. Nami ninajua imeandikwa hivyo. Imeandikwa hivyo kwa kusudi fulani. Yesu alisema hivyo, na akamshukuru Mungu, kwamba Yeye—Yeye alikuwa "ameyaficha kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na angewafunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza." Hilo ndilo kusudi la Mungu katika kufanya hivyo. Yeye . . .

89 Kwa nini akamruhusu mwenye dhambi kuja? Ilimbidi kumwacha mwenye dhambi aje, kwa kusudi la Yeye kuwa Mwokozi. Yeye ni mkuu kuliko dhambi. Yeye . . . kusingalikuwako na dhambi, isingalimbidi kumwacha Shetani kufanya dhambi ya kwanza. Lakini sababu ya Shetani kuiumba ile dhambi ya kwanza, au kuipotosha haki, kuwa dhambi, sababu ya kufanya hivyo, ni kusudi Mungu aweze kuwa Mwokozi. Alimwacha mwanadamu awe mgonjwa, kwa sababu Yeye ni Mponyaji. Naye hana budi kuwa mwenye haki, Naye hana budi kuuweka Mti wa Uzima na mti wa mauti mbele ya kila mtu, kama alivyowafanyia Adamu na Hawa, la sivyo alikosea alipouweka mbele ya Adamu na Hawa. Sasa ni juu yako.

90 Sasa angalieni Imani, Imani ya kweli, Imani halisi, "Imani." Sasa tuchukue makanisa yetu siku hizi, tuangalieni sisi, waangalie watu wetu wa Kipentekoste, waangalie watu wetu wa

Kibaptisti, Wapresbiteri wetu, Wanazarayo, Wapilgrim Holiness, na Maskani ya Branham, sisi sote, tuna hatia, kutoishindania kwa bidii Imani ile.

91 Mzozo mdogo unaweza kutokea kanisani, katika Maskani ya Branham. Nipo nyumbani. Ninaweza kuzungumza juu yenu sasa. Nao wataunda kikundi kidogo, na mmoja ataingia upande mmoja na mwingine upande mwingine. Je, huko ni kuishindania Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja? Je, hilo linasikika kama Fundisho la kimitume? Hapana, bwana, ndugu. Walikuwa na kisa cha Anania na Safira. Mungu angali ni Mungu yule yule. Na tumeona hilo likithibitishwa. Hakuna kuishindania kwa bidii.

92 Watu wanatoka nje leo na kusema, "Vema, imani yangu haifundishi miujiza. Wanafundisha kwamba siku za miujiza zimepita." Basi huishindanii ile Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja.

93 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . lundo la ulokole, mimi mwenyewe. Lakini ninaamini ya kwamba kuna karama halisi, ya kweli ya Roho Mtakatifu, nasi tunaishindania Hiyo kwa bidii. Hiyo ni kweli. Tunaamini Hilo. Watakatifu hunena kwa lugha.

94 Wanasema, "Siamini katika uponyaji wa Kiungu." Siamini katika lundo la ulokole. Lakini tunaamini kuna Mungu, kwamba Yeye huwaponya wagonjwa, ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

95 Nimeona mengi yanayoitwa upambanuzi, siyaamini. Lakini najua kweli kuna Roho wa Mungu mwenye upambanuzi, karama ya maarifa, ambaye huita na kunena, na ni mkamilifu kila wakati. Tunaishindania Hiyo kwa bidii, ile Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja.

96 Najua kunazo ndoto, na matumbo yaliyojaa nya—nyama safi, au yaliyojaa kitu kingine, kinakufanya upate jinamizi mbaya. Unaruka juu na kuliita ono.

97 Kuna ono halisi, la kweli la Mungu. Kweli! Mungu aliliahidi. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele." Yeye hufanya hivyo, wala kamwe halishindwi. Biblia ilisema, "Akiwapo mtu miongoni mwenu, ambaye ni wa kiroho, au nabii, na anene; na yale anayosema, yakitimia, basi msikieni, kwa kuwa nipo pamoja naye. Lisipotimia, msimsikie, maana yeye ni nabii wa uongo." Mungu hawezi kusema uongo. Mungu husema ukweli, kila wakati. Na iwe hivyo. Sasa tunaona ya kwamba hiyo ni kweli. Kuna mambo hayo ambayo . . .

98 Mwangalie Paulo, wakati akiwa huko nje usiku huo, matumaini yote yalikuwa yamekwisha, ibilisi akicheka kila shangwe, akitokeza meno yake kila wakati mawimbi yaliporuka na umeme ukamulika, "Nitamzamisha mtume yule kule nje," maskini hiyo meli ya kale, iliyojaa maji. Na siku baada ya siku,

siku kumi na nne mchana na usiku, nyota hata hazikuangaza; na jinsi meli hiyo ndogo ya kale ilivyorushwa-rushwa. Yeye akitembea huku na huku, akikokota mnyororo nyuma yake, kwa ajili ya kuihubiri Injili. Haleluya!

99 Nasi hata hatuwezi kumruhusu mtu yeyote azungumze juu yetu, tusije tukalipuka kama chura mnene aliyepigwa risasi. Daima tunapiga makelele juu ya jambo fulani. Kisha tuseme tunaishindania kwa bidii ile Imani? Maskani ya Branham inahitaji mambo mengi kunyooshwa, kwanza, vivyo hivyo na Wapentekoste, na Wabaptisti, na Wanazarayo. Hiyo ndiyo sababu hatufikii popote, sisi si wanyofu na waaminifu. Hatujawahi kukutana uso kwa uso na Kitu kile pale, ambacho kinatufanya tusitetemeshwe, sikuzote tukiimarika katika Mungu, Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja.

100 Maskini madumadu wa kale akaingia, na parare, na kuila. "Siku zote za miujiza zimepita. Haikubidi kufanya *Hili*. Haikubidi kufanya *Lile*."

101 Ikiwa Mungu alileta tawi Lake la kwanza kutoka kwa Mzabibu huo, lililokuwa tawi la kipentekoste, pamoja na nguvu, maono, mafunuo, uponyaji, utakaso, Roho Mtakatifu, tawi linalofuata litakuwa kitu kile kile. Bila shaka litakuwa. Kila wakati . . . kila wakati Mzabibu huo utakapochipusha tawi, litakuwa kabisa kama lile lililokuwako hapo mwanzo. Wewe . . . Kama nilivyosema jana usiku, nikizungumza na kikundi cha ndugu: huwezi kuufanya mzabibu uzae maboga. Huwezi kufanya mti wa boga uzae zabibu. Hiyo ni kweli. Uhai wowote uliomo kwenye mzabibu huo, ndio unaozaliwa.

102 Na kama Kristo yuko ndani ya Mzabibu huo, nao Uzima wa Kristo uko ndani ya mtu huyo, utakuwa kama Yesu, utazaa matunda Yake. Ni Roho Wake. Hauwezi kufanya lolote lingine ila kuyazaa. Hauna budi kuzaa Uzima huo, maana ni Uhai ule ule. Kamwe hauwezi kuzaa kitu kingine chochote. Utatenda kama Yeye. Utaongea kama Yeye. Utatembea kama Yeye. Utaponya kama Yeye. Utaona maono kama Yeye. Utazaa Uhai Wake hasa, kikamilifu, kila wakati, kwa maana ni Uhai Wake.

103 Wewe ni ganda tu. Mwanadamu ni kama tu bomba la maji. Yeye siye Maji; yeye ni bomba tu. Hebu ondoa Maji kwake, atapata kutu. Vema, hiyo ndiyo shida siku hizi. Kuna wengi wetu kupita kiasi wanaoingia kutu, ambao wakati mmoja walikuwa na ujuzi. Acha Maji yaendelee kutiririka, hiyo ndiyo inayoufanya mkondo wa Uhai kuendelea.

104 Nilimsikia jamaa fulani akihubiri wakati mmoja, akasema kulikuwa na nguruwe matopeni, akiyafanya maji kujaa matope. Jambo bora zaidi . . . Biblia inazungumzia hilo. Mwondoe huyo nguruwe matopeni. Hebu shuka hapa chini, chemchemi nzuri, na chini hapa mahali fulani penye chemchemi kubwa zikibubujika, huko juu mlimani; maji yote yamejaa matope,

afadhali uwaondoe nguruwe kutoka humo, maji yapate kuwa safi.

105 Kuna mambo mengi sana tunayopaswa kuyaondoa, kabla Maji hayajatoka katika Chemchemi iliyojaa Damu itokayo katika mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa ndani ya hilo gharika hupoteza madoa yao yote ya hatia, kutojali kwao na kupayukapayuka, na kadhalika.

106 Wahudumu kumi na sita, kwa sababu wanaamini... Waliwazia kwamba niliamini kwamba Mungu alilitunza Kanisa Lake na kulihifadhi Kanisa Lake. Maandiko yalisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu," si yeye anayejifanya analisikia. Huyo ni yule ambaye Mungu ameyafungua macho na masikio yake, kusikia. Hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo mpaka Mungu ayafungue macho na masikio yake. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni, bali tayari amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Itakuwaje kwake? Je, Mungu alisema uongo au alisema Kweli?

107 Mwanadamu yuko sahihi, au, "Loo, unaweza kumpata Roho Mtakatifu na kuokolewa, na kesho unaweza kupotea na kwenda kuzimuni"? Kamwe usiuamini upuuzi huo. Huo ni uongo.

108 Ukipata kamwe kuzaliwa mara ya pili, asili yako yote inafanywa tofauti. Kama mtu amepata kupandwa katika Kristo, na kuukubali Uhai wa Mzabibu, unaopitia kwake, hatazaa maboga tena. Unaweza kumfungia moja, lakini anajua kuna kasoro. Atalala pale na kuugua mpaka yatakapoondolewa kwake. Ni mazito kupita kiasi kwake; humwinamisha karibu sana na ardhi. Anapenda kukua. Huwezi kufunga boga kwenye Mzabibu.

109 Tazameni. Loo! "Kuishindania ile Imani," hiyo ilikuwa "kushindania kwa bidii." Sio tu kuishindania, lakini, "kuishindania kwa bidii," kati ya Uzima na mauti. Tutaliendea lingine. Unaweza kukaa muda mrefu juu ya hiyo.

110 Jambo lingine ambalo tungependa kulizungumzia, ni, upendano wa ndugu umeliwa kutoka kwenye huo mzabibu. Upendano wa ndugu! Yesu alisema, "Hivi watu wote watajua ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipendana, ninyi kwa ninyi."

111 Vema, sasa hebu tuchukue tu mfano. Kama mtu haamini sawasawa na mimi, nitaingia moja kwa moja kwenye kusanyiko lake na kuhubiri pamoja naye, nihubiri tu kile anachoamini, na niendelee moja kwa moja na kuliachilia, maana ninampenda. Kwa matunda yao mnawatambua. Kama hawaliamini, na hawana upendano wa ndugu, wanaondoka, wanapinga, wanaondoka, "Kamwe sitahusika Nalo." Kwa nini usije kwangu na kulizungumzia Hilo? Hujui ninachoamini. Unaona? Inaleta tofauti gani, kwa vyovyote vile, ninachoamini? Ni Yule ambaye ninamwamini: Yesu Kristo. Sijawahi kuondoka kwenye

mkutano, bado, nikiwa na hisia mbaya, nijuavyo mimi. Lakini, mnaona, upendano wa ndugu wote umetupiliwa mbali.

112 Naye Paulo aliliona, Wakorintho wa Kwanza 13, akasema, "Upendano wa ndugu udumu." Lakini upendano wa ndugu umeondolewa. Sasa tazameni. Kila wakati . . .

113 Sasa, sikilizeni kwa makini sasa, tunaingia kwenye chakula kigumu. Kila wakati shetani anapoondoa kitu fulani kutoka mtini, tutasema ganda, huyo mdudu hula hilo ganda, anauzungushia tambara la kujibunia, kupachukua mahali Pake. Hebu zungushia tambara kwenye mkondo wa utomvu wa mti, hautapandisha utomvu kwenye matunda ya huo mti. Hautazaa matunda yoyote. Utadondoka moja kwa moja uanguke ardhini. Na hiyo ndiyo sababu, siku hizi, hatuwezi kuwa na uamsho katika siku zetu, ni mafundisho mengi kupita kiasi ya sharti ya kujibunia. Mkondo wa Uhai hautapitia kwenye tambara chakavu. Utadhoofika, Uhai utashuka moja kwa moja ardhini. Hiyo ndiyo sababu miamsho yetu hushindwa.

114 Kama Billy Graham alivyosema hivi majuzi, alikuwa Uingereza, ambako alikuwa na uamsho mkuu. Na mahali pale pale alipokuwa akihubiria, ilimbidi amwondoe mke wake kwenye hizo bustani kwa sababu wanaume na wanawake walifanyia uasherati humo bustanini. Kulikuwa na shida gani? Vitambara vya kujibunia badala ya ganda lililopandwa na Mungu. Havitaubeba Uzima.

115 Kanisa ambalo limezungushiwa kanuni za imani ya kujibunia, halitapeleka Nguvu za Mungu kwenye matawi. Litasema, "Siku za miujiza zimepita," na kuliangusha kabisa chini ardhini. Amina. Najua mnafikiri mimi nina kichaa; lakini, ikiwa ninacho, niacheni, najisikia vizuri hivi. Mnaona? Litaliangusha Neno la Mungu.

116 Kama Mungu akisema hapa, "Mimi ndimi Bwana. Sibadiliki kamwe."

117 "Vema, amebadilika siku hizi," linasema tambara hilo. Linauangusha chini. Mahali lilipoanzia kwanza ni katika nyakati za mwanzoni, ambapo hawakuwa na madhehebu, naye mwanadamu amejaribu kurejesha udugu kupitia kwa madhehebu. Upendano wa ndugu umekatizwa kwa sababu ya madhehebu.

118 Nionyeshe wakati mmoja ambapo Mungu aliwahi kuwa na shirika ama dhehebu, na kamwe akaliweka Kanisa Lake katika madhehebu, au ambapo dhehebu liliwahi kuinuka ambalo halikuanguka wala halikuinuka tena. Sasa, nimekuwa nikisoma tangu nilipotoka kule juu, juu ya somo lili hili. Nimesoma *Kitabu cha Wafia Imani cha Foxe*. Nimesoma maandishi ya mwanzoni ya Josephus. Nilisoma *Babeli Mbili* cha Hislop. Nimesoma *Nyakati za Mwanzoni* na Pember, loo, na *Waanzilishi wa Nikea*, na kabla tu ya Baraza la Nikea, baada ya Pentekoste.

Na kamwe hapajawahi kuwako na dhehebu ambalo Mungu aliwahi kuliweka katika Biblia. Basi tulipoyaweka na kufanya madhehebu, tulitoka nje ya mapenzi ya Mungu.

119 Parare fulani, anayeitwa "dhehebu," alikula ganda asili la upendano wa ndugu, na kuliundia dhehebu, kwa kulizungushia tambara. Nao Uzima wa Mungu unapanda moja kwa moja kupitia kwenye mashina hapa, Shina na Mzao wa Daudi, unapoanza kupanda juu kupitia kwa Roho Mtakatifu; ndipo dhehebu likasema, "Siku za miujiza zimepita. Sio lazima unene kwa lugha siku hizi. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hakuna uponyaji wa Kiungu. Huo ulikuwa ni kwa ajili ya kizazi kilichopita. Umepita, zamani za kale." Na haya hapa matawi juu hapa, yanateseka, yale matunda.

120 Mti mzuri, wenye afya sio lazima unyunyiziwe. Kwa nini tunanyunyizia tena na tena na tena, kwa uchafuzi wa wadudu? Kwa nini tunafanya hivyo? Ni kwa sababu huo mti hauna afya. Kwa nini hauna afya? Kanuni za imani na madhehebu yamekula mkondo wa Uhai kutoka kwake. Kabisa! Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Wapentekoste, walikula mkondo wa Uhai kutoka kwenye mti huo, wakijaribu kuubadilisha na madhehebu, kuwaleta watu wote chini ya siasa. Mungu hataki tuungane pamoja chini ya siasa na kanuni za imani. Tumeunganishwa pamoja na Roho Mtakatifu, ya asili ya Mungu, huikatilia mbali dhambi ya moyo wetu, na kutufanya sote mmoja katika Kristo Yesu. Hiyo ni kweli, ndugu yangu. Hiyo ni kweli, dada yangu.

121 Hilo lilianza katika nyakati za mwanzoni baada ya kifo cha Kristo, na ufufuo, baada ya kifo cha mitume. Miaka mia tatu baadaye, walileta Baraza la Nikea. Hapo ndipo walipounda dhehebu la kwanza, ambalo lilikuwa ni kanisa Katoliki. Linamaanisha, *katoliki* linamaanisha "ulimwenguni kote." Kutoka kwa Katoliki, kanisa lilitokea Luther; kutoka kwa Luther, akatoka Wesley; kutoka kwa Wesley, ikatoka Pentekoste. Kote kote, maskini—maskini njia za mzunguko, hayo mengine madogo, kama vile, loo, Nazarayo, Pilgrim Holiness, na kadhalika, Baptisti, na hayo yote. Wote walitoka katika hilo, wote wamo kwenye njama ile ile, madhehebu. Wakati Mungu anapolipa kanisa baraka, au kundi la watu, upesi wanajizungushia ua dogo, na hapa ndipo wanapochukulia msimamo wao. Mungu anataka kubomoa kila ua.

122 Nakumbuka nilipoenda Magharibi mara ya kwanza. Zilikuwa ni nyakati za kulima, Kansas, nao walikuwa wakiweka ngano mle. Ningewaona hao maskini makaoboi ambao hawakujua lolote kuhusu trekta au—au chochote kile, au kukuza ngano yoyote. Yote waliyojua ilikuwa ni kuchunga ng'ombe. Nasi tukaenda kuleta magari, na kuweka viwanja vya gofu, na kuvaa suruali hizi ndogo za magotini walizokuwa wakivaa kuchezea gofu, na mambo hayo yote namna hiyo. Ningewaona hao wazee wenye nywele ndefu, nyeupe, zilizoning'inia chini ya

kofia zao, nikawaona wakileta mashine ya kujalidi na mashine ya kulima ngano, na vitu kama hivyo, anaweka mguu wake kwenye tandiko, na kuvuta kofia yake chini. Anapazungushia ua mahali hapo; asingevumilia hilo. Hakujua lolote kuhusu kuzungushiwa ua. Alikuwa kwenye eneo, yeye pamoja na Mungu. Mvi zikining'inia chini ya kofia yake namna hiyo; akilia, machozi. Anaivuta tu chini, kasema, "Siwezi kuyavumilia mambo haya." Anamwendesha kuelekea machweo ya jua.

123 Mungu atusaidie leo hii kuwa na wasafiri ambao hawatavumilia kuwekewa ua na madhehebu na kanuni za imani, na waendeshe kuelekea machweo ya jua; kwa Imani isiyotikisika, ambayo ilikabidhiwa watakatifu mara moja; pamoja na upendano wa ndugu unaovunja kanuni zote za imani na nyua, na kusema, "Sisi ni ndugu. Sisi ni mmoja katika Kristo Yesu. Chochote Mungu asemacho, tunasema 'amina' nyuma Yake." Tupe watu wa aina hiyo.

124 Naam, kanuni za imani! Kisha wakaunda kile wanachokiita Wa—Waanzilishi Waliotangulia Nikea. Walikusanyika pamoja, kwa njia hii wakaunda baraza. Katika hilo baraza lilianguliwa kanisa Katoliki, ambalo linamaanisha "kanisa la ulimwenguni kote," likayararulia mbali makanisa yote madogo ambamo Mungu alikuwa akifanya kazi, na kuwaingiza kwa nguvu katika kanisa moja na dini moja.

125 Wakamfungia maksai kwenye mkono mmoja, maksai kwenye huo mwingine, wakaning'iniza msalaba mbele ya mtu, wakamwambia "ubusu la sivyo...na uiname, ukaipokee dini ya Katoliki," la sivyo wamwelekeze maksai mmoja upande mmoja, na huyo mwingine upande mwingine, na kumrarua. Wakamchukua mwanamke na kuzishika nywele zake na kuziweka kwenye pipa la lami, na kumuuliza kama ataubusu msalaba huu; ama angefanya hivyo, na kuiinamia dini ya Katoliki, ama wangeziwasha nywele kichwani mwake na kumteketeza kabisa. Wawaweke kwenye nguzo na kadhalika. Wawaweke kwenye kile wanachokiita mwanamke wa chuma, wawashindilie vigingi hivyo, wakijaribu kuwafanya waubusu huo msalaba, wakumbatie kile wanachokiita "dini ya Kikristo," kisha wawasage wakawa mavumbi.

126 Wafia imani walisimama pale bila kuyapepesa macho yake. Alijua mahali alipokuwa amesimama. Alijua ambaye alikuwa amemwamini. Aliweza, akijua Hili, ya kwamba Mungu angeweza kumfufua katika siku ya mwisho, maana Yeye aliahidi hilo. Kabla hajaisujudia maskini mikondo ya matambara machafu ya kale ya kujibunia, angefia kwenye hicho kisiki. Haleluya!

127 Jalia nifie mahali papo hapo. Mungu wangu asipokuja katika kizazi changu, nitakufa juu ya kile kisiki kilicholiwa na parare, nikiamini ya kwamba Yesu Kristo na Kanisa Lake

na Neno Lake ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Huenda nisiweze kulizaa, katika matawi haya yote, kwa sababu maskini mikondo ya utomvu hapa nje, ya madhehebu na kanuni za imani, yalinikatilia mbali na kuniangusha kama kiazi moto. Hiyo inaweza kuwa kweli. Lakini nitasimama mwaminifu kwenye hicho kisiki na kulia, kwamba, "Saa yaja, Mungu atalirejesha Kanisa Lake, mpaka kwenye hali Yake ya mwanzoni."

128 Hili linaweza likaudhi. Jambo la tatu. Sitaki liudhi. Tazameni mojawapo wa mikondo mikubwa ya utomvu waliokata. Na kwenye wakati huo wa madhehebu, huo ndio ulioharibu mkondo wa utomvu, kwanza kabisa. Jambo la kwanza, kama wangekuwa na upendano wa ndugu mmoja na mwenzake, kamwe wasingelihitaji dhehebu. Na ndipo walipoona wasingeweza...Hawangekuwa na upendano wa ndugu, au walifikiri hawakuwa nao. "Wale wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya." Badala ya kuchukua Neno la Mungu, walikuwa na dhehebu.

129 Luther alitoka kwenye dhehebu hilo. Miaka mia tano na hamsini baadaye, akaondoka. Alifanya nini? Waligeuka moja kwa moja, wakafanya jambo lile lile walilofanya. Moja kwa moja kutoka kwa hilo akaja Calvin. Moja kwa moja kutoka hapo akaja Wesley. Moja kwa moja kutoka kwa Wesley wakaja Wabaptisti, Wapresbiteri, wakashuka hadi kwa Wapentekoste. Nao Wapentekoste, baada ya Nazarayo wakaja Wapentekoste. Na baada ya Pentekoste, itakuwaje? Natumaini Kuja kwa Kristo. Maana, Wapentekoste walifanya jambo lile lile ambalo hao wengine walifanya.

130 Ufunuo 12 inasema kwamba wangefanya hivyo. Alikuwa kahaba, nao walikuwa makahaba. Walikuwa "makahaba." Kanisa Katoliki, "yeye," ilisema alikuwa "kahaba," katika Biblia, k-a-h-a-b-a. Wakorintho wa Kwanza 12 ilisema hivyo. Kisha ikasema, "binti zake." Sasa, hawawezi kuwa ni wanaume. Kamwe hakusema "wanawe." Ilisema, "binti zake." Makanisa yanawakilishwa katika Biblia kama wanawake. Nao binti zake walikuwa ni makahaba, mnaona, jambo lile lile. Aina gani? Naam, vipi, kahaba? Wakifanya uasherati wa kiroho dhidi ya Neno la Mungu. Wakishikilia tambara la kidhehebu badala ya kuishindania Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu, linasema, badala ya kurudi na kulichukua Neno la Mungu.

131 Nilizungumza na kasisi hapa si muda mrefu uliopita. Akasema, "Sijali Biblia inasema nini. Sisi ndio kanisa."

Nikasema, "*Hilo* ni Neno la Mungu."

Kasema, "Tulilifanya."

132 Nikasema, "Mbona libadilike sana hivyo? Hamna hata kitu kimoja kanisani mwenu, ambacho Biblia hii inasema, ambacho mnafundisha." Nilikuwa nikimwambia nilimbatiza msichana mmoja kwa Jina la Yesu Kristo.

Akasema, “Unajua, kanisa Katoliki lilikuwa likifanya hivyo.”

Nikasema, “Lini? Hiyo hapo kila historia ya makanisa, niijuayo, imewekwa papo hapo.”

Akasema, “Tunaamini katekismo yetu.”

Nikasema, “Vipi kuhusu historia?”

133 Kasema, “Hatujali historia ilisema nini. Tunaamini katekismo.”

134 Nikasema, “Unajuaje kulikuwako na George Washington na Abraham Lincoln? Ulijuaje kulikuwako na wale wazee waanzilishi?”

“Kwa sababu tunaamini historia yetu.”

135 Nikasema, “Hakuna mahali ambapo kanisa Katoliki liliwahi kuunda dhehebu mpaka miaka mia tatu na sitini baada ya kifo cha mtume wa mwisho.” Nikasema, “Wala kanisa Katoliki halikujulikana. Hawakubatiza katika Jina la Yesu Kristo, maana walikuwa ndio msingi wa kwanza kabisa wa kuleta ubatizo wa uongo. Nalo ni . . . ”

136 Akasema, “Vema, sasa hebu kidogo.” Akasema, “Tunayo haki. Sisi ndio kanisa. Tunafanya kile tunachotaka kwa sababu Mungu yuko katika kanisa Lake.”

Nikasema, “Mungu yuko katika Neno Lake, si katika kanisa Lake.”

137 Kama kanisa halikubaliani na Neno, basi kuna kasoro fulani. “Neno Langu na liwe kweli, na neno la kila mtu mwingine liwe uongo.” Hiyo ni kweli. Neno la Mungu likiwa ni kweli. Lifanye Neno Lake kuwa kweli. Rudi kwenye Neno Lake. Mnaona kile parare alikula?

138 Sasa, kwenye wakati wa waanzilishi wa mwanzoni wa Nikea. Gene, wewe ulilichunguza tu, pia. Lile Baraza kuu la Nikea lilisababisha ubishi mkubwa, juu ya, “Je, kulikuwako na Mungu mmoja au kulikuwako na Miungu watatu; Baba, akiwa mmoja; Mwana, akiwa wa pili; Mungu Roho Mtakatifu, akiwa wa tatu?” Ndipo wakakubaliana kwamba kulikuwako na “Miungu watatu.” Sasa, kama hamwamini hilo, nitawasomea hilo sasa hivi kutoka katika Baraza la Nikea, Waanzilishi wa Nikea. Walifanya hivyo, “Miungu watatu.”

139 Kuna Mungu mmoja. Kuna Mmoja tu. Yeye ni Yehova Mungu, MIMI NIKO mkuu; Alfa, Omega; Mwanzo na Mwisho.

140 Wamekuwa sasa, kusudi wafanye hivyo, iliwabidi kupata kitu cha kuendana nacho. Kusudi wafanye hivyo, walijaribu kusema, “Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu.” Sasa, kabisa, hakuna kitu kama hicho. Sio Miungu watatu. Huo ni ukafiri.

Kuna ofisi tatu za Mungu yule yule. Ubaba . . .

141 Mungu alipokaa peke yake, mtakatifu; Sheria Zake, haki Yake humfanya mtakatifu. Alitaka kuwa ndani ya mwanadamu. Alitaka kuabudu pamoja na mwanadamu. Alitaka mwanadamu amwabudu Yeye. Ilibidi amjie mwanadamu. Na ndipo alipofanya hivyo, aliumba; akamtia uvuli maskini bikira jina lake Mariamu. Mungu, Yehova alifanya hivyo, na akaumba ndani ya tumbo lake la uzazi seli, seli ya Damu. Seli hiyo ya Damu ilikuza seli nyingi, nayo ikamzaa Mtu, aliyekuwa ni Kristo Yesu.

142 Mungu Mwenyezi, Baba, alikaa ndani Yake. Kwenye ile siku ya ubatizo, alipompokea Roho Mtakatifu kwenye siku ile Yohana alipombatiza, Yohana alisema, "Nilitazama nikamwona Roho wa Mungu, kama Hua, akishuka kutoka Mbinguni, na Sauti ikisema, 'Huyu ni Mwanangu mpendwa ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.'" Yesu alisema kwamba Mungu alikuwa pamoja Naye, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anakaa ndani Yangu." Si Yesu, na kuwa mmoja na Mungu; lakini Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

143 Nanyi ndugu wa Umoja, wengi wenu mnaiendea njia mbaya mnapojaribu kuwazia kwamba Mungu ni mmoja kama vile kidole chako ni kimoja. Hawezi kuwa Baba Yake Mwenyewe. Hawezi.

144 Lakini Yeye ni Mungu. Mungu ni Yehova, yule Roho; Kristo alikuwa ndiye nyumba alimoishi. Ndipo akautoa uhai huu, na, alipofanya hivyo, akamtoa Roho. Na kupitia kwa Damu hii isiyoghoshiwa aliyoimwaga, alinitakasa, apate kuja Mwenyewe na kukaa ndani yangu na ndani yako. Basi Mungu yu pamoja nasi. Huyo ni Roho Mtakatifu, ambaye ni yeye yule, Mungu yeye yule, Yehova Mungu. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Na mambo nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya."

145 Hapo ndipo madumadu walianza kula, parare, wakijaribu kumfanya "Mungu Baba" ameketi Utukufuni, "Mungu Mwana" ameketi mkono fulani wa kuume alio nao.

146 Mkono wa kuume wa Mungu, ambapo Biblia ilisema, "Nikatazama juu na kumwona Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu," Filipo, au Stefano alipopigwa mawe. Haimaanishi kwamba Mungu ana mkono wa kuume, naye Yesu amesimama juu ya mkono Wake wa kuume. Inamaanisha kwamba Yeye yuko katika mkono wa kuume wa Nguvu, mamlaka. "Nimepewa mamlaka yote Mbinguni na duniani," alisema Yesu. Alikuwa katika mamlaka. Mungu alikuwa ndani ya Kristo. Yuko ndani—ndani Yake. Biblia ilisema, "Ndani Yake unakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili." Unapojaribu kufanya Miungu watatu binafsi, wewe ni mpagani kama wapagani wawezavyo kuwa.

147 Sasa, hili litaumiza. Nne. Walipokuwa na miungu watatu, iliwabidi kumwakilishia ubatizo, kwa ajili ya miungu wao watatu, kwa hiyo ibilisi akayapofusha macho yao, kwa Mathayo 28:19, "Enendeni basi, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Mkiwafundisha kushika chochote nilichofanya. Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Ibilisi aliyapofusha macho yao kwa Hilo.

148 Sasa shikilieni hilo. Sasa hapa ndipo sina budi kupigilia msumari, na itaumiza, lakini nawatakeni msikilize. Ni Ukweli. Mungu atusaidie iwe . . . Wewe yachunguze tu Maandiko. Tafuta katika Biblia ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa kwa Jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," tafuta mahali pamoja mtu yeyote alipowahi kubatizwa. Angalia, unasema, "Ibilisi anaweza . . . " Ibilisi huchukua Maandiko hayo na kuyafanya yaonekane kama kitu yasicho.

149 Hivi yeye hakumwambia Yesu jambo lile lile? "Imeandikwa, 'Atakuagizia Malaika Zake, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.'" Kamwe hakujikwaa mguu Wake katika jiwe. Lakini ibilisi alikuwa akijaribu kumfanya aone jambo ambalo Maandiko hayakusema.

150 Alikuwa mwerevu. Alijazwa na Mungu. Mungu alikuwa ndani Yake. Naye Mungu, akiwa ndani ya mwanadamu, ataufanya ufunuo Wake ujulikane. Hakika.

151 Nitawapeleka kwenye Mathayo 28:19, "Enendeni basi, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu."

152 Sasa angalieni jinsi waamini miungu watatu wasio na kadiri kutoka kanisa Katoliki . . . Kamwe hapakuwapo katika Biblia, kamwe hakukuwako na kanuni ya imani ya wazee waliotangulia Nikea, wazee wa—waliotangulia Nikea. Walibatizwa, kila mmoja wao, kwa Jina la Yesu Kristo, kila mmoja wao. Lilipitia kwenye kanisa Katoliki, likatoka kule likaingia kwenye kanisa la Kiprotestanti.

153 Sasa, unawezaje kuliona bila Mungu kulifungua jicho lako? Huwezi. Ninaomba ya kwamba Mungu atayafungua macho yenu kwenye Hili. Basi sikilizeni tu kwa makini sasa.

154 Sasa nitayachukua Maandiko yenu, Mathayo 28:19, "Enendeni, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu."

Ulibatizwaje, "Kwa jina la Baba, katika jina la Mwana, katika jina la Roho Mtakatifu"? Hilo hata halijaandikwa katika Maandiko. Nami ninataka mtu fulani . . .

155 Unasema, "Utatu mtakatifu uliobarikiwa." Nitafutie neno "utatu" popote katika kurasa za Biblia ya Mungu. Ni mpango uliobuniwa na mwanadamu, tambara kuukuu chafu la kanisa

lililozungushiwa humo, kupachukua mahali pa Mkondo wa utomvu wa Roho Mtakatifu wa Mungu. Hakuna kitu kama hicho. Hakuna kitu kama hicho. Kitafute kisha unijie. Unawajibika kufanya hivyo, kama Mkristo, ukikipata. Hakimo katika Maandiko Matakatifu ya Mungu. Nalo "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" limeanguliwa kutoka kuzimu, hakuna kitu kama Miungu watatu.

156 Sasa, ninaamini katika Ubaba wa Mungu. Ninaamini katika Uwana wa Mungu. Ninaamini katika kipindi cha wakati cha Roho Mtakatifu wa Mungu. Lakini ni Mungu yeye yule katika kila wakati, si Miungu watatu.

157 Sasa, "Kwa Jina la Baba." Biblia haikusema, "Enendeni mkabatize kwa jina la Baba, jina la Mwana, jina la Roho Mtakatifu." Ilisema, "Enendeni mkabatize," Yesu alisema, tukiangalia nyuma, "Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Sio "jina la Baba, jina la Mwana," hilo lingewafanya kuwa watu binafsi, lakini sivyo. "Kwa Jina la Baba, na. . ." *Na* ni kiunganishi, na kiini chao kile kile. "Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu." Sio "kwa jina la Baba, jina la Mwana, jina la Roho Mtakatifu." Lakini, "Katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Mnaona? Sasa angalieni.

158 Hawa hapa wamesimama mitume waliotiwa mafuta wakipanda kwenda Pentekoste, kumpokea Roho Mtakatifu. Walienda moja kwa moja hadi Pentekoste na kumpokea Roho Mtakatifu. Sasa, Kanisa limezinduliwa, tutafanya nini? Jambo la kwanza linalotokea, Maagizo hayana budi kutolewa. Daktari Simoni Petro hana budi kuandika Maagizo ya kwanza, kwa sababu Yesu alimpa kalamu. "Nakupa ufunguo, Petro. Lolote utakalofunga, Maagizo utakayoandika hapa duniani, nitayapokea kwenye Duka la Dawa. Andika haya, nami nitayakubali."

159 Walifanya nini? Wale watu waliposikia kelele hizo zote zikitolewa namna hiyo, walisema, "Hii ina maana gani?" Wengine, wakinena kwa lugha. Walisema, "Tunayasikia matendo ya ajabu ya Mungu."

160 Petro alisema nini? "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

161 Sasa walifanya nini? Waliongeza "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" hapa, ambayo hayapo kwenye yale Maagizo. Hiyo ni kweli. Waliongeza nini tena? "Sio lazima utoke na kutenda kama walivyotenda. Hayakupi furaha na nguvu, na kunena kwa lugha, na mambo haya yote. Sio lazima uwe nayo. Fanya tu maungamo yako, peana mkono." Hiyo ni kasumba nyingine ya ibilisi iliyo na sumu zaidi. Kama iliwafanya watende hivyo walipoitumia hiyo Dawa, itakufanya utende vivyo hivyo. Chukua Maagizo Yake sawasawa kabisa.

"Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu."

162 Sasa kumbukeni, kama hapakuwapo na mtu aliyewahi kubatizwa, katika Biblia, kwa njia nyingine yoyote ila kwa Jina la Yesu Kristo, Wayahudi na Mataifa, na watu wa nje na kadhalika, ilibidi wote waje na kubatizwa kwa Jina la Yesu Kristo. Ninampa changamoto mtu yeyote kunionyesha mahali ambapo mtu mmoja aliwahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," au kwa miaka mia tatu baada ya—ya kifo cha mtume wa mwisho. Mbona, ni dhahiri kuliko vidole vyangu kumi mbele yangu. Huwezi kuliona mpaka Mungu ayafungue macho yako. Vema, huo, kama huo si ufunuo sahihi, basi kwa nini Petro, akiwa na ufunuo ule ule, aligeuka moja kwa moja nyuma . . . Siku kumi baada ya Yesu kumwambia, "Nendeni mkabatize kwa Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," Petro akageuka moja kwa moja, akasema, "Mbatizwe kwa Jina la Yesu Kristo, kila mmoja wenu." Basi huu hauna budi kuwa ndio ufunuo ule ule aliopata. Nalo kanisa huko nje, nalo litakuwa la utatu, limepata ufunuo mbaya, basi hawatumii ule Mkondo wa utomvu. Walichukua tambara na kulizungushia pale, nalo linadondosha Uzima wa Mungu pale. Itamuua mgonjwa! Loo, ni mambo mangapi zaidi tungeweza kuyaendea, katika kanuni zenu za imani na kadhalika, yale ambayo imefanya!

163 Hebu nilielezee hili dhahiri tu. Nawatakeni muingie na kuzichukua Biblia zenu kwa dakika moja tu, hivyo basi tunaenda kulifanya rahisi sana watoto watalielewa. Fungueni Mathayo, mlango wa kwanza. Mna Mathayo 28:19. Nendeni kwenye Mathayo, mlango wa kwanza, kifungu cha 18.

164 Tazameni hapa, ninawatakeni mwangalie kwa makini, *huyu* ndiye Baba, upande wangu wa kushoto, *huyu* ni Mwana, katikati, *huyu* ni Roho Mtakatifu, upande wa kulia. [Ndugu Branham anatumia vitu vitatu kuelezea—Mh.] Sasa, Baba ya Yesu Kristo ni nani? Mungu, Baba. Je, hiyo ni kweli? Ninyi nyote mnaamini hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Hakika ninaamini. Mungu, Baba, ndiye Baba wa Bwana Yesu. Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.

165 Sasa ninanukuu Maandiko. Tazameni, unaweza kulichunguza ukienda nyumbani, au ulichunguze sasa. "Sasa kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi . . . " Mathayo 1. Tazameni hapa, kama ambavyo nimesema mara nyingi, kama unasoma kitabu cha hadithi, nawe usome huko nyuma, uchukue tu Mathayo 28:19 namna hii, katika kitabu cha hadithi, "Yohana na Mariamu wakaishi kwa furaha baadaye." Yohana na Mariamu ni akina nani? Rudi mwanzoni mwa hicho kitabu uone Yohana na Mariamu ni nani, kama Yeye alivyosema, "Basi, enendeni, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza kwa Jina la Baba."

166 Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Je, "Baba" ni jina? [Kusanyiko linasema, "Hapana."—Mh.] Hakika siyo. Kwa Jina la

"Mwana." Basi "Mwana" ni jina? ["Hapana."] Ni cheo, kama vile tu "Baba." Je, "Roho Mtakatifu" ni jina? ["Hapana."] Hapana, ni cheo. *Roho Mtakatifu* ni kile Yeye alicho.

167 Unasema, "Roho Mtakatifu ni jina." Na *binadamu* pia. Tazama, mimi ni mwanadamu, lakini jina langu sio "binadamu."

168 Hicho ndicho alicho. Ni Roho Mtakatifu. Hilo silo Jina Lake; hicho ni kile Yeye alicho. Basi ikiwa "Baba" si jina, "Roho Mtakatifu" si jina, wala "Mwana" si jina, basi Jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" lilikuwa ni lipi? [Kusanyiko linasema, "Bwana Yesu Kristo."—Mh.] Bila shaka! Bila shaka! Sasa, unaona, "Baba" si jina.

169 Yesu alisema, "Enendeni mkawabatize kwa Jina la Baba, la Mwana, la Roho Mtakatifu." Petro akageuka moja kwa moja, akasema, "Ni Jina la 'Yesu Kristo.'" Sasa, huo ndio utaratibu hasa walioufuata katika Biblia nzima.

170 Sasa walifanya nini? Watafsiri wao, au watu wa kanisa wamefanya nini? Mashirika yamefanya nini? Walilizungushia tambara la kale la kimadhehebu, wapate kupendwa na hao wengine. Ikinilazimu kula biskuti za magadi na kunywa maji ya umande, na kuifia imani, nitaitetea Kweli ya Mungu na kufia kwenye kisiki. Hiyo ni kweli. Hakuna mtu, papa wa Rumi, ama hakuna askofu wala kadinali, anayeweza kustahimili Hilo. Naam, bwana. Kuna nini? Yaliyosazwa na tunutu, yaliyosazwa na Methodisti, yameliwa na Baptisti. Yaliyosazwa na Baptisti, yameliwa na Pentekoste. Ni—ni—ni mahali pa namna gani! Mikondo yote ya Uhai imekwisha. Hili ni jambo dogo tu.

171 Sasa, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni Nani? "Enendeni basi, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." "Baba" sio jina, "Mwana" sio jina, "Roho Mtakatifu," hakuna jina.

"Unazungumzia Jina gani?" Vema, hiyo ni kama Yohana na Mariamu, hebu turudi nyuma ili kujua ilikuwa nini.

"Sasa kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mama Yake Mariamu alipokuwa ameposwa na Yusufu kabla ya yeye . . . kabla hawajakaribiana, alionekana ana Mimba ya" (Nini?) "Roho Mtakatifu."

172 Nilifikiri mlisema Mungu alikuwa ndiye Baba Yake. Mungu anawezaje kuwa Baba Yake, na Roho Mtakatifu awe Baba Yake? Sasa mnaona, ninyi wa utatu, ati mnawapigia kelele wa Umoja? Nyani haoni kundule. Angalieni hapa, la. Mnaona ninachomaanisha?

173 "Baba." Yeye alisema, kwamba, "Kuzaliwa kwa Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mama yake, Mariamu, alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana Mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu." Basi, "Mungu Baba" hakuhusika nayo? Iwapo—iwapo Mungu Baba, na Mungu Roho Mtakatifu,

si Mtu Yule yule, basi Yesu alikuwa na baba wawili, basi Mwokozi wetu alikuwa mtoto haramu, aliyezaliwa na roho mbili mbalimbali, au kwa roho mbili mbalimbali. "Kuzaliwa kwa Yesu Kristo kulikuwa, Yeye alichukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu." Je, mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi Mungu Baba, na Roho Mtakatifu, ni Roho Yule yule, la sivyo Yeye alikuwa na baba wawili.

174 "Haya yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na nabii wa Bwana, akisema, 'Tazama, bikira atachukua Mimba, naye atamzaa Mwana, nao . . . Mwana, nao watamwita Jina Lake'" (*huyu* Ndiye) "'YESU, aliye Imanueli,' yaani, likifasiriwa . . . " Kitu gani? [Kusanyiko linasema, "'Mungu pamoja nasi.'"—Mh.] Basi Jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni lipi? ["Bwana Yesu Kristo."] Bila shaka. "Ataitwa Jina Lake" ["'YESU,'"] "maana atawaokoa watu Wake na dhambi zao."

175 Sasa, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni nani? Bwana Yesu Kristo. Jina Lake ni lipi? Si jina . . . "Baba" si jina, "Mwana" si jina, "Roho Mtakatifu" si jina. Bali Yesu Kristo ndiye "Bwana Yesu Kristo," ambalo ni Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, zile ofisi tatu za Mungu zikidhihirishwa katika mwili, katika Mtu mmoja. Haleluya! Ndugu, hiyo ni Kweli. Basi nisaidie, Mungu, nitasimama kwenye Siku ya Hukumu juu ya Hilo.

176 Parare amefanya nini? Ana Mungu Baba juu Mbinguni, Mungu Mwana ameketi *hapa* kwenye kiti cha enzi, na Mungu Ro- . . . Si ajabu hatuwezi kufika popote!

177 Mungu yuko ndani yenu, pamoja nanyi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi ukamilifu wa dahari. Na mambo nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya," si Mtu mwingine, bali Roho Mtakatifu yule yule, Mtu yule yule, Mungu yule yule. Yesu, Bwana Yesu Mwenyewe, alikuwa ni Maskani ambamo Mungu alikaa ndani yake, apate kujidhihirisha Mwenyewe, maana Yeye alikuwa ni Roho. Alikuwa ni Roho.

178 Sasa, Yesu hakuwa wa Milele. Mungu ni wa Milele. Yesu sasa ni wa Milele kwa sababu Mungu ameutwaa Mwili.

179 Kulikuwako na wakati mmoja, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, nilikuwa wa Milele. Mungu aliponiwazia, niliwaziwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, jina langu liliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, na lako pia, kabla hakujawa hata na chembe moja ya mchanga. Ni wangapi wanaojua hiyo ni Biblia? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Mungu aliweka jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu? Basi, katika mawazo ya Mungu, tulizaliwa moja kwa moja katika Ufalme Wake.

180 Siku moja kulikuja mwili kupitia ndoa takatifu, baba na mama yangu. Nao wakanizaa, nami huyu hapa naja, William Branham, nikiwakilishwa katika mwili wa nyama. Sasa

mnanijua kama William Branham, mwanadamu. Mungu alinijua kama William Branham, wazo niani Mwake Mwenyewe, na dhihirisho.

181 Neno ni nini? Neno ni wazo lililotamkwa. Hapo aliponena na kusema, "Na aje," nikaja. Atakaposema, "Na aje tena," nitakuja tena. Naam, bwana. Na kwa hiyo, unaona, wazo; neno ni wazo lililotamkwa.

182 Mungu tayari ametoa Neno, jambo pekee ambalo wazo Lake lilikuwa, na Yeye akalitamka. Anapolitamka, likatokea. "Na iwe," ikawa. Huyo hapo Mungu, Yehova mweza yote, mwenye nguvu zote, mwenyezi. Sasa Yeye anawakilishwa.

Kusudi sasa, wapate kutekeleza jambo hili, iliwabidi kupata ubatizo wa uongo kufanya hili.

Unaona, limefichwa. Ulimwengu haulioni, wala haliwezi kuonekana.

183 Sasa angalieni kwa makini, wakati tukiwa na muda wa kutosha ku—kufunga na kufanyiza mstari wa maombi. Vema. Nilichukua muda mwingi kuliko nilivyodhania, juu yake. Hebu kidogo tu sasa, nina jambo lingine ninalotaka kukwambia.

184 Kwa hiyo, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni Mungu mmoja wa kweli. Analo Jina moja. Jina Lake ni Yesu Kristo. Alizaliwa Kristo Bwana alipozaliwa. Yeye, *Kristo,* maana yake "Yule aliyetiwa mafuta." *Bwana* maana yake ni "umilikaji." Alikuwa "umilikaji" na "Bwana." Ndipo Mungu akashuka na kukaa ndani Yake, ambalo lilimfanya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu pia; Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho; Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi, Shina na Mzao wa Daudi pia; Nyota ya Asubuhi, wa Kwanza na wa Mwisho. Huyo Ndiye. Loo!

185 "Yaliyosazwa na tunutu." Unawezaje kuabudu usipojua unachokiabudu? Unawezaje kuwa wa kiroho ispokuwa una Roho Mtakatifu ndani yako? Kama umefungwa kabisa na lundo la kanuni za imani za kanisa, zitakufanya utende kama watu wa kanisa, na—na muungwana na wa kidini, na mambo kama hayo. Hayo yote ni matendo mema, ya kimaadili.

186 Lakini, ndugu, huna budi kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu halisi anayekuja tu kwa Neno la Mungu. Nalo Neno la kweli la Mungu, linapokuja ndani yako, litadhihirisha Kweli. "Yeye, Roho Mtakatifu, atakuja. Atanishuhudia Mimi. Ataidhihirisha ile Kweli. Atayachukua mambo ambayo nimewaonyesha, awaonyeshe mambo ambayo nimesema, naye atawaonyesha hayo. Roho Mtakatifu atawaonyesha." Yale atakayofanya, Yeye huyo hapo.

187 Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu. Na yaliyosazwa na Katoliki, yameliwa na Walutheri. Na yaliyoliwa na Walutheri, yaliyosazwa, yameliwa na Methodisti. Na

yaliyosazwa na Methodisti, yameliwa na Pentekoste. Imefikia wapi? Mkusanyiko huu wote wa dhambi, mambo haya yote, mafundisho, mambo mengine tungeweza kusema, loo, jamani, kupeana mikono, kunyunyizia maji.

188 Ni nani aliyepata kusikia juu ya kunyunyizia? Nionyeshe hilo katika Biblia. Nani aliyesikia juu ya kumwagiliwa maji? Nionyeshe hilo katika Biblia. Ubatizo ulikuja, neno *baptizo,* ambalo linamaanisha "kuzikwa na kufunikwa." Kweli. Hiyo ni Kweli ya Neno la Mungu. Loo, laiti tungalikuwa na wakati, tungeweza kuendelea na kuendelea na mambo ya uongo.

189 Ninasema hivi, watu wangu wapendwa. Nisikilizeni. Nitasimama pamoja nanyi siku moja kwenye Siku ya Hukumu. Itanibidi kujibu. Sitajibu kamwe juu ya kanuni ya imani. (Kwa hiyo nisaidie, Mungu!) Nitajibu kwa Biblia. Hicho ndicho Kitabu nitakachosimama nacho.

190 Hakuna mahali katika Biblia ambapo waliwahi kumpokea Roho Mtakatifu bila kuwa na hisia, kunena kwa lugha, na kupaza sauti, na sifa za Mungu, na unabii, na madhihirisho. Hawakwenda tu na kupeana mikono na mhubiri na kuondoka.

191 Hakuna mahali katika Biblia walipopata kupokea, walipowahi kubatizwa, nje ya kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

192 Kamwe hapakuwapo na mahali katika Biblia walipowahi kufundisha utatu. Sikuzote ilikuwa ni "Mungu mmoja." "Sikieni, Ee Israeli, Mimi ndimi Bwana, Mungu wenu, Mungu mmoja! Usiwe na miungu wengine mbele Zangu. Mimi ndimi Bwana Mungu wako." Sio Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, bali "Mimi ni Mungu!" Milele, Yeye ni Mungu! Daima alikuwa Mungu. Daima atakuwa Mungu.

193 Na wakati madhehebu yatakuacha, unapokuja kwenye kusanyiko na kujaribu kuonyesha upendano wa ndugu, hata pamoja na madhehebu yao, kujaribu kuokota na kuokoa kile unachoweza, kuwavuta ndani, kumwacha Mungu awachukue hao wengine. Na kwa sababu kwamba unasimama juu ya Kweli za Biblia, wanakutenga. Haiwezi kuwa chochote ila hila za kishenzi za ibilisi, kuwazuia watoto wasiingie kuuona mkutano na kuokolewa. Hiyo ni kweli.

194 Huo hapo Mwamba imara wa Neno la Mungu. Nitamchukua mtu yeyote, wakati wowote wanaotaka, na kwenda pamoja nao katika upendano wa ndugu, nami nataka unionyeshe jambo moja ambalo nimesema ambalo si Kweli ya Biblia. Naam, bwana. Ni kweli. Sasa, kwa sababu ukilitetea, unatengwa. Natarajia iwe hivyo. Mungu alisema itakuwa hivyo.

195 Walimtendea vivyo hivyo. "Ulisomea wapi? Ulitoka shule gani? U nani Wewe, Mfarisayo au Msadukayo?" Yeye alikuwa Mwana wa Mungu aliye hai, hakuchukua upande na yeyote wao.

196 Basi nisaidie, Mungu, jalia niwe na ujasiri wa kutosha, jalia niwe na msimamo vya kutosha, jalia niwe mwanamume vya kutosha, nijalie niwe Kristo vya kutosha, kusimama peke yangu (nikisimama, sina budi kusimama hivyo) na kusema Kweli, na kusimama. Naam, bwana. Afadhali niihubiri Injili kwa watu watano, kuliko kuwa na mamilioni wanaosikia. Niseme Ukweli. Kamwe sijawahi kupatana. Nilitaka jambo hili, kwa maana Mungu alikuwa ameniambia ishara hizi kuu na mambo ambayo yanatolewa, kama dhihirisho la kufufuka Kwake, na kadhalika, ni kwa ajili ya Kanisa. Maskini watu hao huko nje, nao wamefungwa katika kanuni hizo za imani na kadhalika, wameshindiliwa mambo sana, kama kutiwa dawa wasioze.

197 Mungu aubariki moyo wako. Sitakuacha katika hali hiyo. Nitakuambia kile Mungu alichosema, "Lakini nitawarudishia yote yaliyoliwa na madumadu, yote yaliyoliwa na parare, yote yaliyoliwa na tunutu. Nitarudisha, asema Bwana!" Kwa hivyo nisaidie, natoa unabii huu. Kabla ya Kuja kwa Bwana, ile Imani ya kweli ya kimitume, yale Mafundisho ya kweli ya kimitume, Roho wa kweli wa Biblia, wa kweli, yuko njiani sasa, akijaribu kula na kupanda juu, kukua tena.

198 Wapentekoste walikuwa naye, kwanza kabisa. Walifanya nini? Walichora mviringo mdogo Kwake, wakaanza kujiundia dhehebu. Naye akaukatilia mbali. Hiyo ni kweli kabisa. Hizi hapa zinakuja, wakati Bwana alipotuma karama hizi, maskini karama nyenyekevu alizonipa mimi. Wanaendelea kuja, wanataka niwe wa kule kumwagika kwa mvua ya masika; waliliundia hilo dhehebu. Wanataka nije nikajiunge na Assemblies.

199 Nimesimama papo hapo katikati ya kila tawi linaloning'inia huko nje, papa hapa kwenye kisiki cha huo Mti, na kusema, "Huu ndio Msingi. Kateni maskini mikondo hii ya vitambara hapa, Uhai uweze kuingia ndani yenu, ndipo mtakuwa na unabii, mtakuwa na upambanuzi, mtakuwa na Roho, mtakuwa na nguvu. Mtakuwa na urejesho wa Kanisa la kweli, mtakaporejea kwenye Mzabibu wa kweli na Uzima wa kweli."

200 Haiwezi kupitia kwenye tambara linalolidondosha chini moja kwa moja, na kusema, "Ilikuwa siku nyingine. Ni siku nyingine." Ni sawa milele. Yeye ni Alfa na Omega; Mwanzo na Mwisho. Kabisa. Itabidi mrudi kwenye ule Msingi, kwa kuwa, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda."

201 Mungu awabariki, marafiki. Najua mnafikiri kidogo nina kelele sana, kidogo nje ya utaratibu, lakini sivyo. Nafikiri niko katika utaratibu pamoja na Neno hili.

202 Ro—Roho wa Mungu yuko hapa, Roho yeye yule aliyeiandika Biblia. Ikiwa Roho aliyeiandika Biblia, atasema "amina" kila wakati Maneno ya Biblia yanaposemwa. Iwapo, *pale*, kila mtu

alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo, Roho wa kweli wa Mungu atasema, "Amina. Hiyo ni Kweli." Nayo Biblia ilisema, "Yesu Kristo, ni yeye yule jana na hata milele," "Nitakuwa pamoja nanyi sikuzote, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari," Roho wa kweli wa Mungu atasema, "Amina." Na ikiwa huyo ni Roho wa kweli wa Mungu, basi nguvu za kweli na madhihirisho ya Roho yatajidhihirisha Yenyewe pamoja na huyu Roho wa kweli. Lihukumuni Neno mnalolisikia. Lihukumuni kwa Biblia. Yatazameni matendo Yake. Zitazameni kazi Zake.

203 Je, kuna watu hapa wanaotaka kubatizwa, ambao hawajawahi kubatizwa, wanaotaka kubatizwa? Inua mkono wako. Sawa.

204 Kama hakuna mabatizo basi, sawa, basi tutawaombea wagonjwa. Je, kuna mtu yeyote hapa ambaye ni mgonjwa? Inua mkono wako, unayetaka kuombewa. Ni wangapi hapa ambao ni wageni miongoni mwetu, nao wanataka kuombewa; Sikujui, wala hatufahamiani, sikujui? Vema. Wagonjwa na wanaoteseka, siwajui ninyi.

205 Ikiwa Mungu ni Mungu, kama Yeye ni Mungu wa Neno ninalohubiri; Yesu alisema, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya." Je, hiyo ni kweli? Yesu alisema, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya. Mengi kuliko hayo mtayafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba." Ilikuwa ni nini? Kugeuka kutoka kwa Mwanadamu, mwili, kurudi kwenye Nguzo ya Moto tena. Paulo alipokutana na Yeye akienda zake Dameski, Yeye alikuwa ni nini? Nguzo ya Moto. Hiyo ni kweli? Bila shaka alikuwa. Yeye ni nini leo? Yeye ni nini kwenye picha *ile*?

Unasema, "Loo, unaweza *kusema* hivyo, Ndugu Branham."

206 Kama hiyo kweli ni kweli ya Mungu, endapo ni Nguzo ile ile ya Moto, Yesu Kristo yeye yule, ninadai Roho Wake akiingia ndani yangu, atafanya jambo lile lile alilofanya Yeye. Atakubaliana na kila Neno alilosema, haidhuru madhehebu yatakariri kanuni zipi za imani. Atanena Neno Lake. Alilinena Hilo.

207 Kutokuamini kwao hakukumzuia. Kanuni zao za imani na madhehebu, Yeye kamwe hakuchukua upande wowote na yeyote wao. Alihubiri Injili isiyoghoshiwa ambayo alikuwa ameisikia kutoka kwa Mungu. Alisimama peke yake. Hakika, Yeye alisimama. Pale Kalvari, hapakuwapo na hata mtu mmoja ambaye angesimama karibu Naye. Alisimama peke yake.

208 Ikiwa wewe utakuwa chochote, utamtetea Mungu, utasimama peke yako. Ni wewe! Sio ulimwengu, sio kanisa lako, sio dhehebu lako. Ni wewe, kati yako na Mungu. Sijali yale . . .

209 Maskani ya Branham wanaweza kufanya watakayo. Nataka wamwamini Mungu; nataka waje. Lakini wasipokuja, sitapatana nao katika jambo lao duni. Nitamtetea Mungu.

210 "Methodisti. Utafanya nini, Ndugu Branham? Wa—Wapentekoste wa utatu?" Nilithibitisha kuwa ninawapenda. Nimewaendea, na kutuma kwenye Assemblies of God na church of God.

211 "Na kama Waumoja, nyinyi mnabishana na Waumoja kwa sababu ya yule 'mmoja' wao, anayesimama, namna hiyo." Naam, bwana. Yesu alikuwa na Baba. Alikuwa Mungu. Wanabatiza katika Jina la "Yesu." Ninabatiza katika Jina la "Bwana Yesu Kristo." Kuna akina Yesu wengi, lakini kuna Bwana Yesu Kristo mmoja tu. Mnaona? Sio kwa Jina la "Yesu." Lakini kwa Jina la "Bwana Yesu Kristo," huyo ni Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.

212 *Bwana,* "Bwana alimwambia Bwana Wangu, 'Keti mkono wa kulia.'" Mwana, *Yesu. Kristo,* Logos aliyetoka kwa Mungu, hapo mwanzo. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Haya basi.

213 Loo, nimelifurahia sana! Moyo wangu unafurahi tu! Na kujua ya kwamba Roho Wake, Roho aliyeliandika Neno, anakubaliana na Neno, anathibitisha ule mkondo wa Uhai. Anaingia, anajidhihirisha Mwenyewe. Mungu awe nanyi. Ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Nimesema Kweli kuhusu Neno Lake.

Sasa ninyi, ninyi watu wa maskani, ninawaombea wakati mwingine. Tumechelewa. Nilikuwa nimepita kidogo, nikapitisha wakati kidogo. Nilikuwa nikitarajia wengine wabatizwe.

214 Tazama. Ikiwa Roho Mtakatifu yuko hapa, tutaninii . . . Yeye ataninii—Yeye atawaponya. Nataka wale watu ambao ni wageni malangoni petu, walio—walio wagonjwa na wanaoteseka. Na sasa kama nimesema Kweli kuhusu Mungu, na watu hawa walisema kweli, kwamba siwajui, nao ni wagonjwa na wanateseka; ikiwa Roho Mtakatifu angali yeye yule, anaweza kunifunulia. Ikiwa huyo ni Roho Mtakatifu yeye yule, na ameunganishwa na kisiki kile kile *hapa* chini ambacho parare wamekula, lakini kuna kipande kidogo cha ganda kinachopitia *pale* chini, kinachounganisha hili pamoja, kitafanya kazi kama tu kilivyofanya huko chini.

215 Kanuni za imani za kanisa zitasema, "Loo, hiyo si sawa. Hiyo ni telepathia ya kiakili. Huyo ni i—ibilisi. Huko ni kupiga ramli."

216 Walisema vivyo hivyo juu Yake. "Ikiwa wanaita Bwana wa nyumba 'Beelzebuli,' ni zaidi sana jinsi gani watawaita wanafunzi Wake?" Kweli. Bado hiyo hailikomeshi. Hiyo huliongeza tu, hulifanya liendelee.

217 Sasa, Yeye angali ni Mungu? Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Yeye huliheshimu Neno Lake? Huliheshimu.

218 Nami ninamshurutisha kila mmoja wenu, kama hujawahi kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, batizwa katika Jina la

Yesu Kristo. Sijali kile tambara la kale la kanisa lisemacho. Hiyo ni dhehe-. . .

219 Nami ninajua watu niliowaleta moja kwa moja kwenye chumba changu cha kusomea, na kusoma. Nikiwa karibu na watu wazuri, ningesema, "Njoni hapa kwa dakika moja. Hebu nionyeshe ambapo ulibatizwa kwa jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,' kama hilo ni la Kimaandiko."

220 Na anapobanwa kabisa, anasema, "Ninajua hilo, Ndugu Branham, lakini usimwambie mtu hili kunihusu." Unaona?

221 Nikasema, "Litetee fundisho lako, nionyeshe ambapo mmoja. Kila mtu katika Biblia, wao . . . "

222 Wengine wanabatiza, bila jina hata kidogo, iliwabidi waje wakabatizwe tena, kabla hawajampokea Roho Mtakatifu. Ni wangapi wanaojua hilo? Paulo alipitia pwani ya juu ya Efeso, akakutana na Wabaptisti. Walikuwa na nanii mzuri . . . Walikuwa na mchungaji mzuri. Alikuwa mwanasheria aliyeongoka, Apolo. Naye akawaambia, "Je, mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

223 Wakasema, "Hata hatujui kama kuna Roho Mtakatifu."

224 Kasema, "Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?" Inasema katika King James, "mlibatizwaje." Isome katika ile ya asili, inasema "vipi." "Mlibatizwaje" ni mamoja. "Mlibatizwa namna gani?"

225 Wakasema, "Tumebatizwa kwa Yohana, mtu yule yule aliyembatiza Yesu." Huo ni ubatizo mzuri. "Akatoka majini, yeye yule aliyebatiza . . . Yohana."

226 Vema, Paulo alisema, "Huo hautafaa tena. Huo haufai tena. Amekwisha kuja, amesulubiwa. Sababu Yohana alibatiza kwa toba, si ondoleo la dhambi, akisema mnapaswa kumwamini Yeye ajaye, Yesu Kristo." Basi waliposikia hili, walitoka wakaingia majini na kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo. Paulo akaweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao. Wakatabiri na kunena kwa lugha. Hiyo ni kweli? Paulo aliwalazimisha watu waliokuwa wamebatizwa na mtu yule yule aliyembatiza Yesu, akawaambia itawabidi kubatizwa tena, kwa sababu hawakubatizwa katika Jina la Bwana Yesu.

Ninayo haki ya kusema jambo lile lile. Ni Fundisho lile lile.

227 Sasa, Paulo alisema nini katika Wagalatia 1:8? Sasa, alifanya hivyo. Ni wangapi wanaojua hiyo ni Kweli? Semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naye akasema, "Kama Malaika kutoka Mbinguni," sembuse mhubiri kutoka kwenye kanisa au dhehebu! "Kama Malaika kutoka Mbinguni akija na kuwahubiri injili yoyote isipokuwa Hii, na alaaniwe. Kama nilivyosema hapo awali, nasema tena, ijapokuwa sisi au Malaika kutoka Mbinguni atawahubiri injili yoyote isipokuwa Hii ambayo mmeisikia tayari." Mnaona mahali ambapo

parare wameula wote? Mnaona? “Lakini kama Ma—Malaika akiwahubiri jambo lingine lolote isipokuwa Hili lilivyo, na awe kwenu aliyelaaniwa.” Hiyo ni kweli. Na alaaniwe. Msimsikilize hata kidogo.

228 Na kama mchungaji, kama mmishenari, kama mwi—mwinjilisti, au mtu yeyote, akijaribu kuwalazimisha mbatizwe kwa njia nyingine yoyote isipokuwa katika Jina la Yesu Kristo, hebu niseme pamoja na Paulo, “Na alaaniwe.” Mtu yeyote akikwaambia, “Peana mikono na mhubiri nawe utampokea Roho Mtakatifu,” na alaaniwe. Kwa maana, Roho Mtakatifu ni Kuzaliwa. Wanamtaka kwa njia yao wenyewe.

229 Mtu yeyote anajua, nilisema hapo awali, kuzaliwa ni machafuko, sijali kuko wapi. Kama kuzaliwa kumo kibandani, ni machafuko. Kama kuko ndani ya nyumba, ni machafuko. Kukiwa hospitalini, katika chumba cha waridi, kilichopambwa, ni machafuko. Kuzaliwa daima ni machafuko.

230 Na Kuzaliwa upya ni vivyo hivyo hasa. Ni machafuko; kulia na kupiga mayowe, mguno tu, midomo yenye kigugumizi, na makelele ya kila namna. Ni machafuko, lakini huleta Uzima. Njia pekee ambayo unaweza kuifanya.

231 Kamwe usichukue kupeana mikono, au kuweka jina lako kwenye kanisa fulani, kupanda juu na kusema, “Ninamwamini Mungu Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi; na Yesu Kristo, Mwanaye; kanisa Katoliki takatifu la Kirumi; na ushirika wa watakatifu.” Ukifanya hivyo, unashuhudia kuwa wewe ni mwana mizimu.

232 Chochote kinachoshirikiana na wafu, sijali ni nini, ni ibilisi. “Kuna Mpatanishi mmoja tu kati ya Mungu na wanadamu, huyo ni Mwanadamu Yesu Kristo.” Naye hajafa, bali Yu hai. Naye yuko hapa sasa; alifufuka katika wafu. Watakatifu wengine wote wa Kikatoliki na watakatifu wa Kiprotestanti, na wowote wale, wamekufa na wako kaburini. Wanaweza kuwa Utukufuni. Kama walikuwa watakatifu, wako Kule. Sijali walipo, kama ukishirikiana nao, unavunja sheria za Mungu kabisa na unapitia kwa ibilisi. Sio mtakatifu. Bila shaka. Biblia ilisema hivyo.

233 Tunutu alikula hilo, pia, lakini Mungu ataurudisha kwa Roho wa kweli wa Mungu aliye hai, ambaye hawasiliani na Yuda Mtakatifu fulani, na Mtakatifu *Huyu*, na Mtakatifu *Yule*, na Mtakatifu Sisilia, na hawa wengine wote, na baadhi ya watakatifu hawa. Itakuwa ni Roho wa Yesu Kristo ambaye atarudi na kujidhihirisha Mwenyewe na kufanya jambo lile lile. “Nitarudisha, asema Bwana.” Nami namshukuru Mungu, leo hii, juu ya tawi la Kanisa *hapa* juu, kuna Uhai mdogo unaoanza kupenyeza Mle. Anajidhihirisha Mwenyewe. Mungu atalirudisha Kanisa kamili kwenye kimo Chake kinachofaa tena, kabla ya Kuja kwa Bwana.

234 Bwana Yesu, hii ibada ni Yako. Ninawajibika tu kwa Neno, kulihubiri. Sasa limefanywa. Liko mikononi Mwako, Bwana. Ninaomba ya kwamba katika Jina la Kristo, ya kwamba utayapokea mambo haya, na katika nuru ambayo yamehubiriwa, Bwana. Naomba, ikiwa dhamiri yoyote imeumizwa, na iponywe kwa Zeri ya Gileadi. Jalia hao, Bwana, wanaoketi hapa ambao wamenyunyiziwa, wakamwagiliwa, ama kuzamishwa katika miungu watatu, jalia waone kosa lao, Bwana. Naweza . . . haidhuru ningehubiri kiasi gani.

235 Wakati ulipohubiri na kufanya jambo lile lile, na hata hivyo macho yao yalipofushwa. "Hakuna mtu anayeweza kuja kwangu asipovutwa na Baba Yangu." Na ingawa ulikuwa umehubiri na kufanya miujiza, na kuthibitisha ya kwamba Wewe ulikuwa Masihi, hata hivyo wasingeweza kuamini, kwa sababu Isaya alisema ya kwamba watakuwa hivyo.

236 Nami huenda nikaongezea hili, ya kwamba, leo, ingawa umefanya mambo mengi sana, umelitoa Neno Lako la kweli, ukalirudisha katika msingi wa kimitume, ukaliweka chini kwa changamoto, ya kwamba ni Kweli, ndipo unarudi moja kwa moja nyuma Yake na kufanya miujiza kama uliyofanya ulipokuwa hapa duniani. Inakuwaje? Hawawezi. Kwa sababu, Paulo alisema, kwa Roho (kama Isaya alivyosema), "Watakuwa wakaidi, wenye majivuno, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiopenda kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wenye kuwadharau walio wema; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake. Hao nao mjiepushe nao."

237 Bwana, ninaomba leo kwamba utajidhihirisha Mwenyewe na—na kufanya ninii Lako—kufanya Neno Lako liishi kati yetu sasa hivi. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Kama utafanya hivyo, Bwana, wote wataamini. Tutatembea kutoka kwenye maskani hii asubuhi ya leo, tukiamini ya kwamba nafsi yetu imekombolewa, ikiwa tu Wewe (naamini) utaituma kwao, Bwana, na kuzungumza na kila moyo, huku tukiutazamia upambanuzi Wako.

Jalia Roho Mtakatifu, Uzima wa kweli wa Mungu, aje katika sehemu hii ndogo ya tawi lililosalia. Ee Bwana, litie nguvu kwa Roho Wako. Jalia . . . Inashuhudia, Bwana. Kushuhudia, Neno Lako ni la kweli. Kila mtu ni mwongo; Wewe ni Ukweli. Haijalishi ni wangapi watakaoupinga; kama itachukua ufia imani, ikihitaji kutengwa na ushirika, ikihitaji kufanya miamsho, kufikia ambapo inabidi umchukue mtu mmoja tu na kusimama juu ya . . . Hao watoto maskini wa Mungu, watatoka, kwa vyovyote vile, haidhuru. Watakuja, kwa vyovyote vile, kusikia.

238 "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu, mgeni hawatamfuata." Sauti Yako, jinsi ilivyowaita kondoo Wako kwa mara ya kwanza, inaita tena. Na mgeni hawatamfuata. Kama

Sauti Yako, iliyowaita kondoo Wako, ilisema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo,” Kondoo wako waliisikia. Kondoo wako wanasikia jambo lile lile leo hii. Ikiwa mmoja alisema, “Loo, hayo ni—hayo ni mambo ya upinga Kristo. Ubatizwe, jina la ‘Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,’” mgeni hawatamfuata. Wataijua Sauti Yako. Watayatazama matendo Yako. Ninaomba, Baba, ya kwamba utayajalia yote. Sauti Yako imenena, kazi Zako na zifuate. Katika Jina la Yesu. Amina.

[Ndugu mmoja ananena kwa lugha—Mh.] Sasa, rafiki, Roho Mtakatifu akitenda kazi.

239 Sasa nitalipa kusanyiko hili kisogo. Sasa, siwataki ninyi watu mlio hapa kwenye maskani hii, afadhali niangalie *huku*, sitaki mtu yeyote wa maskanini; ninakutaka wewe ambaye hujawahi kuwa hapa awali, au unajua kwamba sikujui. Watu wa nje ya mji, inueni mikono yenu tena, ambapo ninaweza kuona mahali mlipo, ya kwamba ninyi ni wagonjwa. Hebu Roho Mtakatifu asogee sasa. Sasa, kwenu ninyi watu, siwajui.

240 Je, mna kadi za maombi? Je, walisambaza ninii zozote za maombi . . .? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . wamegusa.

241 Na umwache afanye hivyo angalau mara mbili. Biblia ilisema, “Katika kinywa cha . . .” Ni mashahidi wangapi? “Wawili ama watatu.” Je, hiyo ni kweli? “Mashahidi wawili ama watatu, kila neno na lithibitishwe.” Tuchukue angalau wawili au watatu kati yenu, kisha wengine wenu muamini. Chochote unachohitaji, wewe kiamini sasa hivi.

242 Je, utafanya hivyo, kama Yeye atalifanya? Inua mkono wako, useme, “nita—nita—nitalichukua kwa imani, nainua tu mkono wangu.” Je, utafanya hivyo? Inueni mikono yenu, kila mtu humu ndani. Ni wangapi humu ndani wanaosema, “Sijawahi kuliona hapo awali. Nitalichukua kwa imani, pia”? Inua mkono wako, useme, “Nitalichukua kwa imani.” Angalia hapa.

243 Sasa unaona mahali ninaposimama? Hapa kuna changamoto. Sasa, iwapo Yeye ni Mungu, atajidhihirisha Mwenyewe. Kama hii si Kweli, basi mimi ni mwongo na nabii wa uongo. Hupaswi kamwe kuja kunisikiliza tena, kwa sababu mimi ni nabii wa uongo; ninatoa ushuhuda wa Kristo usio wa kweli. Huwezi kulifanya na kuthibitisha fundisho nililokuwa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

244 Wewe njoo. Unatoka hapa, maskanini, sivyo, mama? Wewe unayeketi hapo umeinua mkono wako, umevaa kofia ndogo nyeupe. Naam. Unatoka hapa. Unaona, ninapoiona hiyo hapo, watu wanavuta ono hilo. Ninaweza kuiona ikisimama moja kwa moja juu yao.

245 Lakini ninasubiri mtu ambaye simjui. Hapa, wewe unayetoka maskanini hapa, mama ambaye umeinua leso yako *hivi*, unayeketi papa hapa? Je, unatoka . . . Wewe, u—unatoka nje

ya mji? Simama kwa miguu yako kwa dakika moja. Ulipokuwa umeketi pale, ukiomba, kulikuwa na hisia fulani isiyo ya kawaida iliyokujia, kwa ghafla. Huyo alikuwa ni Malaika wa Bwana. Sasa Yeye amesimama karibu nawe sasa. Sasa kuna kitu, ambacho umemgusa Yeye. Sijui ni nini. Lakini wewe umetoka nje ya mji. Inawezekana umetoka Louisville, au Tennessee, au popote unapoweza kuwa. Sijui. Mungu anajua hilo. Lakini kama atanifunulia kile wewe. . . siri ya moyo wako, akujulishe sha—shauku yako, au chochote kile, utaamini, ukikubali Neno, ukifanya kila kitu kama tu. . .

246 Sasa ninyi watu wote, mnaomwangalia moja kwa moja huyo mwanamke, tutaona. Sasa hebu Roho Mtakatifu, kama angali ni Roho Mtakatifu, hebu alifunue. Usiogope. Yeye ni Mungu. Yeye hutimiza Neno Lake, kila Neno.

247 Huyu Mwanamke amerukwa na akili, ugonjwa wa neva. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Una ugonjwa wa moyo, pia. Huo ni moyo wenye fadhaa. Unakuuma zaidi unapolala, unakusonga roho zaidi. Umefanyiwa upasuaji. Upasuaji huo bado haujapona. Hiyo ni kweli. Sivyo? La, hutoki Ohio. . . Unatoka Ohio. Unatoka Ohio. Naam, bwana. Una mzigo moyoni mwako. Ni msichana fulani, au kitu fulani. Ni binti, amepotea. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Nenda, pokea ulichoomba, mama. Uligusa kitu Fulani. Unaamini?

Ni nani wengine waliokuwa wameinua mikono yao. . .? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . hapa ndani?

248 Unaamini Mungu anaweza kunifunulia siri ya moyo wako? Unaamini ni Mungu yeye yule nimekuwa nikimhubiri asubuhi ya leo? Una kivuli cheusi juu yako, ni kansa. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaamini? Vema, bwana, basi rudi Ohio unakotoka, Lebanon, rudi ukaponywe, ukimwanini Bwana Yesu Kristo. Nenda, amini.

249 Maskini mama huyu anayeketi papa hapa, kwa namna fulani. . . Ana namna fulani ya upele wa ngozi. Simama, mpenzi. Unaamini? Kwa namna fulani ilikushtua kidogo, sivyo? Vema. Ni. . . Utakuacha. Utakuwa mzima. Ninakuona, baadaye. Nenda nyumbani, uwe mzima.

250 Ni nani mtu huyo aliyesimama dakika chache tu zilizopita? Mtu fulani huko nyuma alisimama, mahali fulani. Wewe uliyeinua mkono wako juu, simama kwa miguu yako. Unaamini Yesu Kristo anaweza kuniambia shida yako ni nini? Unalikubali? Unaamini kwamba fundo hilo litaondoka shingoni mwako? Mke wako ameketi hapo karibu nawe, anasumbuliwa na fadhaa. Hiyo ni kweli, pia. Nyote mnatoka Ohio. Weka mkono wako juu yake hapo, ndugu.

251 Bwana, jalia waponywe, warudi nyumbani kwao, wafurahi na kuponywa, kupitia Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

252 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .mtu fulani karibu na wewe. Lichukueni Neno langu; ninawaambia Neno la Mungu. Mnaliamini sasa? Wote wanaoamini, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."] Neno limedhihirishwa. Ni Ukweli.

Sasa inamisheni vichwa vyenu.

253 Bwana, ninakuja Kwako katika Jina la Yesu, nikiwaombea watu hawa. Muda umeenda sana, Bwana. Na kweli imechelewa kuliko tunavyodhania. Ni Kuja kwa Bwana, kumekaribia. Tunaomba kwamba rehema Zako zitaongezewa. Wape, Bwana, uponyaji wao. Sasa ninamhukumu ibilisi, kwa Nuru ya Neno la Mungu; kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwamba ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo ndio sahihi. . .

*TUNUTU, NZIGE, PARARE, MADUMADU* SWA59-0823
(Palmerworm, Locust, Cankerworm, Caterpillar)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 23 Agosti, 1959, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org